Kuelewa Biblia
Ratiba ya uanafunzi-Sehemu ya 4
Na Dennis Dickinson 2020

# Mafunzo ya Huduma: Wachungaji, Wainjilisti, Mamishonari

Na wale wanaohitaji zaidi!

**Karibu** - kwenye mafunzo ya welewa wa Biblia,sehemu ya 4-Shule ya mafunzo ya Biblia. Elisha alipoenda kujifunza chini ya Eliya,alimwita baba.Paulo alimwita Timotheo mwanawe (Timotheo wa pili 1). Wale waliojifunza maandishi ya manabii waliitwa wana wa manabii. Neno mwana katika Kiebrania linamaanisha kujenga. Walijenga maisha yao juu ya walichojifunza. Alikuwa Samweli aliyeanzisha shule ya manabii (kumbuka kwamba ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa kizazi cha manabii katika Matendo ya Mitume 7). Wakati shule za manabii zilifungwa katika siku za za giza za Ahabu (Wafalme), waelekezi walihamia mapangoni na wana wao (wanafunzi). Eliya na Elisha walizifungua tena. Walipohitaji jengo kubwa, waelekezi na wanafunzi walilijenga. Ilikuwa kawaida kwa wanafunzi kuishi na walimu wao. Sila, Timotheo, Tito na wengine walikuwa pamoja na Paulo kila alikoenda.Wanafunzi 12 walienda katika nyumba moja na Yesu Kapernaumu. Hapa ndipo unapoingilia!Kanisa lolote lililo na mwalimu mzuri linaweza kufanya yale ambayo yamefanywa mwanzo. Ukiishi katika kijiji cha watu 200, na kuwe na kanisa la 40, na watu 2 wanaopenda kujifunza maswala ya huduma, makala haya yanaweza kukusaidia kufanya hivyo.Kama Ibrahimu, Samweli, Eliya na Elisha, ama shule za mapangoni nyakati za dhiki,unaweza kujifunza na kuwafundisha wengine.

**Jinsi inavyofanya kazi** - Makala yote yametengenezwa kutumika: 1. Darasani. 2. Katika mijadala ya makundi. 3. Katika masomo ya kibinafsi pasipokuwa na mwelekezi. Mijadala ya makundi ambapo kila mtu anashirikishwa, ni bora sana kuliko masomo ya mihadhara.

**Baba (Msimamizi) -** MMtu lazima aangalie mambo. Mtu mmoja ateuliwe kuhakikisha kwamba: 1. Kazi imekamilishwa kwa njia nadhifu tena kwa mpangilio mzuri. 2. Zoezi la kila wiki linapelekwa kwa msimamizi. 3. Kila mtihani unatolewa na majibu ya gredi kurekodiwa.Rekodi zinawekwa jinsi huduma au utamaduni wenu huhifadhi rekodi.Karatasi ya majina ya wanafunzi na rekodi ya: 1. Kozi. 2. Msimamizi (ikiwa yupo). Kozi zingine za kupita ama kuanguka tu na gredi ya 100 ikiwa imekamilishwa.

**Mafunzo na Muda wa Darasa(Saa ya dakika 50) -** Kila koziinahitaji saa 6 kila wiki na saa 3 na mwelekezi au mijadala ya makundi. Iwapo hakuna mwelekezi au mijadala ya makundi kwa kozi,zile saa 6 za masomo zitakuwa 9. Kila kozi ichukuwe masaa 140 kwa jumla. Saa 6 za masomo na saa 3 za mafunzo na 3 za darasani. Kitabu chako cha msingi ni Biblia.Maelekezo yako ndani ya makala. Tanbihi: Iwapo mchungaji hana mafunzo, anaweza anaweza kufanya kazi kupitia kwa makala akiangaliwa na watu 2 au 3ambao wanaweza kutia sahihi Cheti au Stashahada(au Shahada katika nchi ambazo inaruhusiwa) Iwapo uko kwenye chuo na utumie makala haya, ni sawa na mafunzo mazima 3 kila moja ikitumia mfumo wa Marekani (mafunzo mazima 3 inamaanisha saa 140 za kozi nzima ambayo huhusisha masomo yoyote ya darasani) Kwa mwanafunzi anayesoma muda mzima kozi 5 za wiki 13-15 (kozi moja ya huduma) inakamilisha sehemu ya 1 ya msimu wa masomo. Kozi 10 hukamilisha mwaka. Tarehe za mafunzo hutolewa kulingana kulingana na hoja ya utamaduni na nchi yenu. Wengine hufuta kalenda ya masomo ya nchi husika. Kumbuka kwamba unamiliki na kuendeleza Kituo cha Mafunzo ya Bibla.

**Kwa mwendeshaji wa ratiba** - Yesu alianza na kutamatisha na wanafunzi wote 12. Yohana Marko alishindwa kukamilisha alichoanza, na hivyo safari iliyofuata ya Paulo hakutaka kwenda naye, ila baadaye akasema alikuwa amekua kuwa mtu wa maana. Chagua wale watakaokamilisha walichoanza.Vitu vingine viwili: 1. Wanafunzi wasiosoma kwa muda mzima wanaochukua kozi 1 au zaidi nyinginezo wazingatie muda mahususi kikamilifu. 2. Iwapo kuna wengine wasiosoma vizuri, zingatia ratiba mbadala ya ziada inayoruhusukipindi cha niezi 12 badala ya ile ya 9. Hakikisha kuwa kuna mapumziko ya wiki moja katikati ya muhula wa masomo.

**Kwa wanafunzi** - Dakika 50 ni za masomo. Pata muda wa zoezi ambapo unaweza kunywa maji mengi kukuwezesha kufikiri.Unaweza kumaliza siku yako ya masomo ukipenda. Masaa matatu kabla na masaa 3 baadaye. Madarasa mengine huchukua muda mrefu na mengine mfupi. Pamoja yasawazishe muda wako. Tia bidii and ufanye kazi njema kwa maana unamfanyia Mungu wako kazi!Saa za huduma zinaweza kusambazwa, au kukamilishwa kwa siku. Yote inategemea aina ya huduma. Kusafisha, kuanzisha, kufundisha watoto au masomo ya Biblia, Ushuhuda, kusaidia familia, au huduma nyingine katika mji wako. Ni lazima upate ruhusa kutoka kwa mtu anayeendesha ratiba (wanaweza pia kuwa nza kitu kingine kwa ajili yako) Madarasa ni wiki 12-15.

**Kwa Waelekezi** - Wakati mwingine kunaweza kuwa na kazi nyingi kwa mwanafunzi kukamilisha katika mafunzo yake ya kila wiki. Ni lazima kufanya mabadiliko panapohitajika lakini uhifadhi ubora wa kazi yenyewe.

**Mwaka 1 Stashahada kwa masomo ya Biblia**
**Awamu 1 (wiki 15)**

Welewa wa Agano Jipya Sehemu 1
Welewa wa Agano la Kale Sehemu 1
Mafunzo ya Kimsingi(Masomo)
Ushauri na Uanafunzi
Huduma 1 (saa 6-9 kila wiki)

**Awamu 2 (Wiki 15)**

Welewa wa Agano Jipya Sehemu 2
Welewa wa Agano la Kale Sehemu 2
Tabia na mpango wa milele wa Mungu
Injili ya Yohana, Waraka wa 1,2,3 wa yohana
Huduma 2 (saa 6-9 kila wiki)

**Mwaka wa 2 Sawa na Shahada Shirikishi**
**Awamu 3 (Wiki 15)**

Luka Mtakatifu (au nyingine)
Warumi (au nyingine)
Wahebrania na Filemoni
Waefeso, Wafilipi, Wakolosai
Huduma 3 (saa 6-9 kila wiki)

**Awamu 4 (Wiki 15)**

Matendo ya Mitume
Wakorintho 1 , 2
Timotheo 1, 2 na Tito
Kanuni za Huduma
Huduma 4 (saa 6-9 kila wiki)

**Zoezi na Jinsi ya kusoma kila kozi ya Agano Jipya:Biblia ni kitabu chako cha marejeleo**

Utasoma sura 1-2 kila wiki kwa kila kozi. Soma sura mara 5 (na mara 10 ikiwezekana) na ujibu maswali: Nani? (mtu mmoja au zaidi, wa kiume, au kike), nini? (kinafanyika), lini? (wakati uliopita, uliopo, ujao) wapi? Kwa nini? Vipi? orodhesha amri au maswali yoyote, mambo ya kufanya au kutofanya, na mrejelewa au mlengwa wa maneno hayo. Hakikisha unaelewa kila neon. Hatimaye kwa maneno yako mwenyewe andika makala mafupi juu ya mafundisho ya kila sura. Peana karatasi yako. (Baadhi ya sura ni ndefu sana na kwa hivyo baadhi ya mazoezi yatakuwa yamefupishwa (ikiruhusiwa) iwapo haitakamilishwa kwa wakati kwa mwanafunzi mzuri, peana kazi yako kamilifu kila wiki.

**Kozi ya agano jipya**

**Mathayo** (sura mbili kila wiki)
**Marko** (sura moja kila wiki, 15-16 pamoja)
**Luka** (sura mbili kila wiki)
**Yohana Mtakatifu, 1, 2, Waraka wa 3 wa Yohana** (sura mbili kila wiki)
**Matendo ya Mitume** (sura mbili kila wiki)
**Warumi** (sura moja kila wiki,15-16 pamoja)
**Wakorintho wa kwanza na pili** (sura mbili kila wiki)
**Wagalatia 1, 2 Wathesalonike** (sura moja)
**Waefeso,Wafilipi,Wakolosai** (sura moja)
**Timotheo wa kwanza, Timotheo wa pili, Tito** (sura moja kila wiki)
**Waebrania, Filemoni** (sura moja kila wiki)
**Yakobo, Waraka 1 wa Petro, Waraka 2 wa Petro, Yuda** (sura moja kila wiki)
**Ufunuo wa Yohana** (sura mbili kila wiki)

**Huduma ya kila wiki**

Huduma 1, 2 , 3, 4 (au zaidi) – Huu ni muda wa masaa 6-9 kwa wiki katika kuhudumu, kufunza au huduma.

**Uelewa wa biblia ya Agano Jipya na Kale 1, 2**

Katika uelewa wa kozi za Bibilia, utasoma agano jipya mara 12 na Agano la Kale mara 6. Hii itakusaidia kuelewa bibilia. Kujifunza kupitia kusoma kitu mara nyingi imetumika kwa muda mrefu kwa masharti. Endelea na mwendo na usisite kutegemea kurasa. Soma tu!kila kusoma kunafaa kukamilishwa kila siku kwa siku sita kwa wiki na itachukua muda wa saa moja unusu kukamilisha iwapo wewe ni msomi bora; kwa hivo usisome polepole. Utasahihisha karatasi ya kumaliza kila wiki. Gredi ni umalizaji wa usomi wote. Tanbihi: kwa wale wasio na Agano la kale, Tumia kozi 2 za Agano jipya.

**Uelewa wa Bibilia ya Agano Jipya 1**

Wiki 1, 2 Yohana Mtakatifu 1-12
Wiki 3, 4 Yohana Mtakatifu 13-21, Waraka wa 1, 2, 3 wa Yohana, Waraka wa kwanza wa Petro
Wiki 5, 6 Waraka wa 2 w a Petro, Wagalatia, Yakobo Wathesalonike wa 1, 2, Luka Mtakatifu 1
Wiki 7, 8 Luka Mtakatifu 2-11

Wiki 9, 10 Luka Mtakatifu 12-24
Wiki 11, 12 Matendo ya Mitume 1-14
Wiki 13, 14 Matendo ya Mitume 14-28
Wiki 15 Marko 1-13

**Uelewa wa Bibilia ya Agano Jipya 2**

Wiki 1 Marko 1-13
Wiki 2, 3 Marko 14-16, Wakorintho wa kwanza 1-16
Wiki 4, 5 Wakorintho wa pili, Timotheo wa 1, 2, Tito
Wiki 6, 7 Warumi, Waefeso
Wiki 8, 9 Waebrania, Wafilipi, Wakolosai, Filemoni
Wiki 10, 11 Mathayo 1-15
Wiki 12, 13 Mathayo 16-28
Wiki 14, 15 Yuda, Ufunuo wa Yohana

**Uelewa wa Bibilia ya Agano la Kale 1**

Wiki 1 Mwanzo 1-29
Wiki 2 Ayubu
Wiki 3 Mwanzo 30-Kutoka 4
Wiki 4 Kutoka 5-29
Wiki 5 Kutoka 30- Mambo ya Walawi 13
Wiki 6 Mambo ya Walawi 14- Hwsabu 6
Wiki 7 Hesabu 7-26
Wiki 8 Hesabu 27-Kumbukumbu la Torati 13
Wiki 9 Kumbukumbu la Torati 14- Yoshua 7
Wiki 10 Yoshua 8-Waamuzi 8
Wiki 11 Waamuzi 9-Ruthu-Samweli wa kwanza 8
Wiki 12 Samweli wa kwanza 9, Samweli wa pili 2
Wiki 13 Samweli wa pili 3, Samweli wa pili 24
Wiki 14 Zaburi 1-70
Wiki 15 Zaburi 71-126

**Uelewa wa Agano la Kale 2**

Wiki 1 Zaburi 127-150, Mithali 1-24, Wimbo ulio Bora
Wiki 2 Mithali 25-31, Mhubiri, Wafalme wa kwanza 1-10
Wiki 3 Wafalme wa kwanza 11-Wafalme wa pili 9
Wiki 4 Wafalme wa pili 10, Mambo ya Nyakati wa kwanza 7
Wiki 5 Mambo ya Nyakati wa kwanza 8 ,Mambo ya Nyakati wa pili 8
Wiki 6 Mambo ya Nyakati wa pili 9-36
Wiki 7 Obadia, Yoeli, Yona, Hosea, Amosi, Isaya 1-12
Wiki 8 Isaya 13-46
Wiki 9 Isaya 47-66, Nahumu, Zefania, Yeremia 1-9
Wiki 10 Yeremia 10-35
Wiki 11 Yeremia 36-52, Habakuku, Maombolezi
Wiki 12 Ezekieli 1-28
Wiki 13 Ezekieli 29-48, Danieli 1-4
Wiki 14 Danieli 5-12, Ezra, Hagai, Esta 1-6
Wiki 15 Esta 7-10, Zakaria, Nehemia, Malaki

# Mafunzo na Tafsiri

Peana karatasi yako ya kila wiki ukifupisha Nani, Nini, Lini, Wapi, Mbona na Vipi.Utafanya masomo ya maneno kadhaa na kujifunza kuwa jinsi neno litakavyo tumika litaeleza maana.

**Week 1 Bibilia yatoka wapi?**

Kariri Warumi 3:1-2, Zaburi 147:19-20, Waebrania 1:1-2

**Sehemu ya kwanza**-Maandiko yaWayahudi-Kanisa ya mwazo iliamua kwamba iwapo huwezi amabatanisha nakala moja kwa moja na mmoja wa mitume wa asilli 12 (Shahidi wake na msingi wa kanisa) si andiko.Soma mara tatu Kumbuku la Torati 18:15-22 (18 Atakuwa myahudi), ilikuwaje hakika iwapo Nabii alikosea kwa mstari wa 20, 22. Nabii walipeana ufunuo kutok akwa Mungu. Hakuna fununu au kubahatisha.Iwapo atakosea atakuwa Nabii wa uongo mpaka ile siku atakapofariki. Soma Waefeso 3:1-59 (Kiyunani humaanisha wazi "Mitume ambao ni manabii". Matendo ya mitume 1:8,15-26. Nini kilichohitajika kuchukua nafasi ya Yuda kama mtume na mshuhuda wa ufufuo na mafunzo ya Yesu? na Yohana 15:27, Petro wa pili 1:16, Wakorintho wa kwanza 9:1, 14:37-38 (Kumbuka kuwa mitume wanaweza kuamrisha makanisa). Ni manabii wangapi walikua Wayahudi?

**Sehemu ya pili**-Maandiko ni hewa ya Mungu-maandiko ya hewa ya Mungu yanasema, Timotheo wa pili 3:16. Soma Mwanzo 2:4-7. Nini kinachofanyika Mungu anapo pumua kwa mtu au maandiko? Soma mara mbili Petro wa kwanza 1:16-21, Yohana 15:26-16:15 (Tanbihi 13), Wakorintho wa kwanza 2:1-13. Sura ya 13 Roho Mtakatifu anachukua kile anachokisikia, anatumia fikra na maneno ya mitume, na kutufunza. Kanisa kutoka mwanzoni imetumia maandiko ya Manabii (mitume pia ni manabii) kama chanzo cha ukweli kwa kanisa. Soma Waefeso 2:19-22 hatuongezi kwa msingi.

**Wiki ya 2 Haki,kuwa mwenye haki,kuhukumu**

Wengi hutatizika kuelewa Wokovu (ukamilifu), na kuhesabiwa haki inayofanyika mbele ya hakimu (iliyo sahihi, isiyo sahihi, upatikane na makosa au usipatikane na makosa). Mistari yote iliyo na kila mifano ya neno la Wayahudi kwa kuhesabiwa haki ipo hapa. unaweza hitajika kusoma muktadha kidogo kutathmini jinsi inavyotumika. Tanbihi 5, 5, 5 yamaanisha kuwa neno limetumika mara tatu katika mstari. Andika kwa njia ambayo inatafsiriwa, na uje na maelezo yako ya maana ya maneno; **Mwenyehaki, Haki**; **Mathayo**

**Mtakatifu** 1:19, 3:15, 5:6, 10, 20, 45, 6:33, 9:13, 10:41, 11:19, 12:37, 13;17, 43, 49, 20:4, 7, 13, 21:32, 23:28, 29, 35, 25:37 **Marko** 2:17, 6:20 **Luka Mtakatifu** 1:6, 6, 17, 75, 2:25, 5:32, 7:29, 35, 10:19, 29, 12:14, 57, 13:27, 14:14, 15:7, 16:8, 9,10, 11, 15, 18:6, 9, 11, 14, 20:20, 23:41, 47, 50, **Yohana** 5:30, 7:18, 24, 16:8, 10, 17:25 **Matendo ya mitume** 1:18, 3:14, 4:19, 7:24, 26, 27, 35, 52, 8:23 ,10:22, 35, 13:10, 39, 17:31, 18:14, 22:14, 24:15, 15, 20, 25, 25:10, 11, 15, 28:4 **Warumi** 1:16, 17, 18, 18, 29, 32, 2;8, 13, 13, 26, 3:4, 5, 5, 5, 10, 20, 21, 22, 24, 25, 26, 26, 26, 28, 30, 4:2, 3, 5, 5, 6, 9, 11, 11, 13, 22, 25, 5:1, 7, 9, 16, 17, 18, 18, 19, 21, 6:1, 7, 9, 13, 13, 14, 16, 18, 19, 20, 7:12, 8:4, 10, 30, 30, 33, 9:1, 10, 28, 30, 30, 30, 31, 31, 10:3, 3, 3, 4, 5, 6, 10, 14:17, **Wakorintho wa kwanza** 1:30, 4:4, 6:7, 8, 11, 13:6, 15:34, **Wakorintho wa pili** 3:9, 5:21, 6:7, 14, 7:2, 12, 12, 9:9, 10, 11:15, 12:13 **Wagalatia** 2:16, 16, 16, 17, 21, 21, 3:16, 6, 8, 11, 11, 21, 21, 24, 4:12, 5:4, 5, 5, 17, 21, 21, 3:6, 6, 8, 11, 11, 21, 21, 24, 24, 4:12, 5:4, 5, 5. **Waefeso** 4:24, 5:9, 6:1, 14 **Wafilipi** 1:7, 11, 3:6, 9, 9, 4:8 **Wakolosai** 3:25, 25, 4:1, **Wathesalonike wa pili** 1:5, 6, 9, 2:10, 10, 12, **Timotheo wa kwanza** 1:9, 3:16, 6:11, **Timotheo wa pili** 2:19, 22, 3:16, 4:8, **Tito** 1:8, 2:12, 3:5, 7 **Filemoni** 18, **Waebrania** 1:9, 5:13, 6:10, 7:2, 8:12, 10:38, 11:4, 7, 33, 12:11, 23**, Yakobo** 1:20, 2:21 ,23, 24, 25, 3:6, 18, 5:6, 16, **Waraka wa kwanza wa Petro** 2:23, 24, 3:12, 14, 18, 18, 4:18, **Waraka wa pili wa Petro** 1:1, 13, 2:5, 7, 8, 8, 9, 13, 15, 19, 21, 3:13, **Waraka wa kwanza wa Yohana** 1:9 , 9, 2:1, 29, 3:7, 7, 10, 12, 5:17, **Yuda** 7, **Ufunuo wa Yohana** 2:11, 6:6, 7:2, 3, 9:4, 10, 19, 11:5, 5,1 5:3, 4, 16:5, 18:1, 19:2, 8, 11, 22:11, 11, 11, Soma Warumi 3 mara 5 na ueleze kuhesabiwa haki.

**Wiki 3 Kuokolewa bila kuhesabiwa haki**

Kariri Matendo ya Mitume 4:12. Hapo chini kuna kila mstari ulio na kila neno la aina ya wokovu .Andika chini njia zote tofauti ambapo neno la wokovu limetafsiriwa na uandike fasili yako,Neno Kilatini latamkwa sodzo.

**Sehemu ya 1**. Jina lipi limepewa Masia na mbona,Mathayo 1:21.Sehemu iliyobakia ya Mathayo yaonyesha akiokoa watu wake. Bila kuwahesabia haki au kuwafikisha mbinguni! **Mathayo** 1:21, 8:25, 9:21, 22, 22, 10:22, 14:30, 16:25, 18:11, 19:25, 24:13, 22, 27:40, 42, 27:40, 42, 49. **Marko Mtakatifu** 3:4, 5:23, 28, 34, 6:56, 8:35, 35, 10:26, 52, 13:13, 20, 15:30, 31, 16:16. **Luka mtakatifu** 1:47, 69, 71, 77, 2:11, 30, 3:6, 6:9, 7:50, 8:12, 36, 48, 50, 9:24, 24, 56, 13:23, 17:19, 33, 18:26, 42, 19:9, 10, 23:35, 37, 39. **Yohana Mtakatifu** 3:17 ,4:22, 42, 5:34, 10:9, 11:12, 12:27, 47. **Matendo ya Mitume** 2:21, 40, 47, 4:9, 12, 4:12, 5:31, 7:25, 11:14, 13:23, 26, 47, 14:9, 15:1, 11, 16:17, 30, 31, 27:20, 31, 34, 28:28. **Warumi** 1:16, 5:9, 10, 8:24, 9:27, 10:1, 9, 10, 13, 11:11, 14, 26, 13:11. **Wakorintho wa kwanza** 1:18, 21, 3:15, 5:5, 7:16, 16, 9:22, 10:33, 15:2. **Wakorintho wa pili** 1:6, 6, 2:15, 6:2, 2, 7:10. **Waefeso** 1:13, 2:5, 8, 5:23, 6:17. **Wafilipi** 1:19, 28, 2:12, 3:20.**Wathesalonike wa kwanza** 2:16, 5:8, 9. **Wathesalonike wa pili** 2:10, 13. **Timotheo wa kwanza** 1:1,15, 2:3, 4, 15, 4:10, 16. **Timotheo wa pili** 1:9, 10, 2:10, 3:15, 4:18. **Tito** 1:3, 4, 2:10, 11, 13, 3:4, 5, 6. **Waebrania** 1:4, 2:3, 10, 5:7, 9, 6:9, 7:25, 9:28, 11:7. **Yakobo** 1:21, 2:14, 4:12, 5:15, 20. **Waraka kwanza wa Petro** 1:5, 9, 10, 3:21, 4:18. **Waraka wa pili wa Petro** 1:1 ,11, 2:20, 3:2, 15, 18. **Waraka wa kwanza wa Yohana** 4:14. **Yuda** 3, 5, 23, 25**. Ufunuo wa Yohana** 7:10, 12:10, 19:1, 21:24. Sehemu ya pili-yafwatayo ni neno la wokovu likiumganishwa kwa neno la kufikiri, "fikra iliyookoka**" Marko mtakatifu** 5:15, **Luka mtakatifu** 8:35. **Matendo ya mitume** 26:25, **Warumi** 12:3, **Wakorintho wa pili** 5:13, **Timotheo wa kwanza** 2:9, 15, 3:2. **Timotheo wa pili** 1:7. **Tito** 1:8, 2:2, 4, 5, 6, 12. **Waraka wa kwanza wa Petro** 4:7. Sehemu ya tatu-Andika fasili ulioipatana ushughulikie makala haya tatanishi. Soma **Timotheo wa kwanza** 2:8-15 na ueleze msitari 15. Eleza **Wafilipi** 2:12. Kumbuka kwanza unaushughulikia wokovu wako lakini si kuhesabiwa haki kwako!

**Wiki 4 Amani Na Mungu**

Kariri Wakolosai 2:19-10. Amani katika maandiko na Mungu kila mara ni neno la Kiebrania linalotamkwa: Shalom. Linamaanisha:kulipa gharama, kujaza, kufanya upya, kukamilisha ama kufanya mambo kuwa sawa. Rekodi njia ilivyotafsiriwa na upate fasili ya ni nini maana na kuwa na SHALOM na Mungu. Weka neno SHALOM katika kila msitari na utamke unavyokwenda. Kuna mistari mingi kuorodhesha yote kwa hivyo soma haya kupata fasili. **Mwanzo** 15:15, 29:6, 6, 37:4, 14, 14, 41:16, 43:27, 28, 44:4. Kutoka 18:7, 21:34, 26, 36, 36, 22:1, 3, 3, 4, 7, 11, 12, 14**. Mambo ya Walawi** 6:5, 26:6. Hesabu 25:12. **Kumbukumbu La Torati** 7:10, 23:6, 21, 32:35. **Waamuzi** 11:13, 18:15. **Ruthu** 2:12. **Samweli wa kwanza** 17:18, 22, 25:5, 6, 6, 30:21 **Samweli wa pili** 3:39, 18:29, 32, 20. **Wafalme wa kwanza** 2:5, 6:7, 7:51, 8:61, 11:4, 15:3, 14. **Wafalme wa pili** 4:7, 26, 26, 26, 26, 5:21, 229:17, 20:3. **Nehemia** 6:15. **Mambo ya nyakati wa kwanza** 12:38, 18:10, 28:9, 29:9, 19. **Mambo ya nyakati wa pili** 5:1, 8:16. **Ezra** 5:16, 9:12, **Esta** 2:11**. Ayubu** 9:4. **Zaburi** 29:11 ,31:23, 34:14, 50:14, 56:12, 61:8, 62:12, 66:13, 69:22, 73:3, 76:11, 91:8, 119:165**. Mithali** 6:31, 7:4, 11:1, 13:21, 16:7, 22:27, 25:22**. Mhubiri** 5:4, 4**. Wimbo ulio Bora** 8:10. **Isaya** 9:6, 7, 19:21, 26:3, 12, 34:8, 42:19, 53:5, 54:10, 57:21, 60:20, 65:6. **Yeremia** 13:19 (jumla au yote) 18:20 ,28:9, 29:7 ,7 ,11 , 51:24. **Yoeli** 2:25**. Mika** 3, **Nahumu** 1:15. Zaidi ya mara themanini inatafsiri "dhabihu ya amani," ingawaje neno dhabihu, si la kihebrania.Ni tafsiri ipi uliyoipata? Tumia tafsiri yako kueleza: **Yohana** 14:27, 16:33, **Warumi** 5:1, 8:6, 14:17-19, 15:13, 33, **Waefeso** 1:2, 2:14-17, 4:1-3, 6:15. **Wafilipi** 1:2, 4:6-9 **Wakolosai** 1:2, 20, 3:15.

**Wiki 5 Injili ni nini?**

Kariri Wakorintho wa kwanza 15:22, Warumi 5:12. Ni jinsi gani Walawi walitoa fungu zao za kumi kwa Melkizedeki katika Wahebrania 7:1-10? Paka huzaa paka, wenye dhambi huzaa wenye dhambi. Soma Kutoka 1-2 kisha sura ya 3 mara 5. Andika jinsi dhambi ilivyoingia ulimwenguni. Soma Warumi 5:6-21 mara 5, eleza mstari wa 12. Soma Wakorintho wa kwanza 15:20-28, Yeremia 17:9, Warumi 3:9-31, 6:23, 7:7-8:1. Soma Waraka wa kwanza wa Yohana mara 2 na ueleze jinsi Yohana anavyofunza kuhusu kumjua na kutomjua Mungu.

**Kusulubiwa na Kristo au bila Kristo**: Soma Luka Mtakatifu 9:23, 14:27. Kila mtu yafaa auchukuwe msalaba na aende na Yesu kusulubiwa,au watasulubiwa bila Yesu(kwa mkono wake wa kushoto au kulia). Wagalatia 2:20, 5:24, 6:14, Wakolosai 2:20-3:4. Kuna mistari kwa ishara hizi zote: Taji ya miba kutokana na laana. "Amelaaniwa Yule atakayetundikwa kwenye mti" (Sio mbinguni wala duniani, Ufunuo wa Yohana 20:11). Mkono unaonekana kama ufanyacho. Miguu ni jinsi unavyotembea au kuishi. Kupigwa misumari kwa laana alofanya mwanadamu. Kuumizwa (kupigwa) yatafsiriwa ugonjwa, yaeleza mateso. Moyo ni chanzo cha dhambi zote na ghasia. Giza yamaanisha kuachwa na Mungu. Uchi ni aibu.Kuzimu kulitengenezewa shetani na malaika wake.

**Wiki 6** Rejelea kutumia karatasi zako.Zoezi ni la hiari.

**Wiki 7 Siku za mwisho**

Kariri mistari miwili ya chaguo lako. Chini ni makala makuu ya siku za mwisho. Andika maelezo ya yale unayoyaona. Soma kitabu cha Danieli,falme zake 4, Babiloni, Uajemi, Uyunani na Roma. Sura ya 9 ni miaka ya 70 (wiki ya miaka) au miaka 490. Siku ambayo Masihi atafariki imepewa, soma Mathayo Mtakatifu 24-25, Marko matakatifu 13, Luka Mtakatifu 17, 21, Wathesalonike wa kwanza 5, Wathesalonike wa pili, Timotheo wa pili 3:1-9 (katika kanisa), Waraka wa pili wa Petro 3, Ufunuo wa Yohana. Pitia haya tena iwapo una muda. Kumbuka shuda ya walimu wa uongo.

**Wiki 8 Nafsi = Maisha, Matamanio**

Kariri Ezekieli 18:4. Wahebraniayatamkwa NEPHESH, na Kiyunani PSUCHE.Nafsi ni maisha ya mtu, matumaini na ndoto. Soma na ujaze nafasi hiyo kwa neno, nafsi. Rekodi nija zote neno nafsi limetafsiriwa katika mistari hii na upeane fasili yako. Kutoka 1:20, 21, 34:3, 8, 35:18, Mambo ya Walawi 5:1, 2, 4, 6:2, 17:11, 14. (Kunguni hawana damu kwa hivyo hawana nafsi), nafsi ya waliokufa katika 19:28, 21:1, 11, 26:16, 30, Kumbukumbu la Torati 12:23 ,14:26, 26, v18:6, 19:21, 21:24 (kwa matamanio ya nafsi yake)Samweli wa kwanza 2:33, 35 (mawazo), 18:1, 20:17 Samweli wa pili 3:21, 17:8. Mambo ya Nyakati wa Kwanza 28:9. Ayubu 10:1, 1, 18:4, 32:2 (hali ya maisha), 41:21 (pumzi), Zaburi 10:3, 13:2, 16:10, 27:12, 35:13, 41:2, 63:10, 77:2, 78:18, 88:3, 14, 105:18 (yeye=nafsi), 106:15, 119:28. Mithali 6:16 (yeye=nafsi) 8:36, 11:17, 12:10, 14:10 (hicho=nafsi), 23:2 (hamu) 7 (moyo), 28:22, 31:6 (moyo) Wimbo ulio Bora 1:7, 3:1, 2, 3, 4, Isaya 1:14, 3:20 (Kasha la nafsi-manukato) 53:10, Yeremia 2:234 (raha za nafsi), 15:1 (mawazo), 9, 31:25, 34:16, 51:14, Maombolezo 3:51, 23:17, 18 (mawazo), Mika 7:3. Habakuku 2:5. Mathayo Mtakatifu 6:25, 25, 10:28, 20:28, 22:37, 26:38. Marko Mtakatifu 3:4, 8:35, 35, 36, 37, 14:34. Luka Mtakatifu 1:46, 2:35, 9:56, 12:19, 22, 23, 14:26. Yohana Mtakatifu 10:11, 15, 24 (sisi=nafsi zetu), 25, 27, 13:37, 38. Matendo ya Mitume 2:41, 43, 3:23, 4:32, 14:2 (Mawazo), 22, 15:24, 26, 20:10, 24. Warumi 2:9, 13:1, 16:4. Wakorintho wa pili 12:15 (wewe=nafsi). Waefeso 6:6. Wafilipi 1:27, 2:30. Wakolosai 3:23. Wathesalonike wa kwanza 2:8, 5:23. Waebrania 4:12, 6:9 (nafsi = meli inayombeba binadamu), 10:38-39, 12:3 (Mawazo), 13:17. Waraka wa kwanza wa Petro 1:9, 22, 2:11, 25. Waraka wa pili wa Petro 2:8, 14. Ufunuo wa Yohana 6:9 (nafsi iko kwenye damu), 18:14. Unaelezaje maana ya neno: NAFSI? Yohana Mtakatifu 15:13. Mwanadamu kukata tama ni nini? ubinafsi ni neni linalorejelea wanadamu wa kimwili. Eleza mistari hii na neno ubinafsi ndani mwake. Soma Wakorintho wa kwanza 2:1-3:4 mara 5. Katika sura ya 2:14 (mwanadamu mbinafsi) ni shida. Eleza mbona. Wakorintho wa kwanza 15:44, 44. Soma Yakobo 3:13-18 mara 5 na ueleze 15 na Yuda 19 (hisia=ubinafsi)

**Wiki 9 Roho, mawazo,Fikra**

Unafikiri kwa kutumia roho yako katika maandiko, unapumua, kuwa na mitazamo, na pia inatafsiri utulivu, kupumzika au nusia. Unaposoma, weka neno, ROHO katika mistari kwa sehemu ya vitu vingine kuona jinsi itakavyotoshea. Wahebrania ilitamka: ruach, Kiyunani kikatamka: pneuma. Mwanzo 1:2, 3:8, 6:3, 6:17, 7:22, 8:21 ("kunusia roho tulivu" kauli ya kawaida ya Waebrania) 26:35, 27:27, 27, 27 (kunusa ,27, 27), 41:8, 41:27. Kutoka 5:21, 6:9, 15:8, 15:10, 29:18 ("roho wa utulivu" 25,41,41). Hesabu 14:24, 16:22, Yoshua 2:11. Waamuzi 8:3, 16:9 (kunusia moto). Samweli wa kwanza 1:15, 16:14, 15, 16, 23 (Kuuisha roho) 30:12. Samweli wa pili 22:11. Wafalme wa kwanza 10:5, 18:45, 21:5, 22:23. Mambo ya nyakati wa kwanza 9:24. Mambo ya nyakati wa pili 21:16. Ayubu 7:11, 10:12. Zaburi 18:120, 31:5, 32:2, 51:10, 17, 77:3, 6, 78:8, 104:4, 143:7. Mithali 11:13 ("roho ya amina"), 14:29 ("yeyote Yule aliye na mapua marefu" na "mwenye upungufu wa r oho"), 15:4, 13, 16:2, 19, 32, 17:22 (msongo wa mawazo), 18:14, 14, 25:28. Mhubiri 7:8, 8, 9 ("mrefu wa roho "na "mwenye kimo kirefu kiroho") 8:8, 10:4, Isaya 11:3, 19:3, 14,2 5:4, 29:10, 24, 38:16, 41:29, 54:6 (mwenye msongo wa mawazo), 58:11, (maji ni roho). Yeremia 13:24, 31:12 (maji ni roho) 49:32, 36, 51:11. Maombolezo 4:20. Ezekieli 3:14, 14 (roho moto=hasira), 11:19, 13:3, 18:31. Danieli 4:8, 9, 5:11, 12, 14, 20, 7:15. Hosea 5:4, 9:7 (mtu mwenye roho), Mika 2:11. Mathayo mtakatifu 5:3, 10:1, 20, 26:41. Marko mtakatifu 2:8, 3:11, 8:12, 9:17, 14:38. Luka mtakatifu 1:47,80 (mawazo), 2:40, 4:33 ("roho ya mtu mchafu mwenye fitina"), 6:18, 7:21, 8:2, 29, 10:21, 23:26. Yohana mtakatifu 4:23, 24, 24, 6:63, 63, 11:33, 13:21. Matendo ya mitume 6:10, 7:59, 11:28, 16:16, 17:17 (mawazo), 18:5, 18:25, 19:21, 20:22 (mawazo hutengenezwa). Warumi 1:4, 9, 2:29, 7:6, 8:6, 9, 8:15 (kufikiri, 15), 16, 11:8, 12:11. Wakorintho wa kwanza 2:11 (fikra za mawazo), 12, 4:12, 5:3 (wazo), 4, 5, 6:20, 7:34, 14:15, 15 (matamshi sambamba ya kiyahudi, kusema kitu sawa mbili), 16, 32 (kumbuka mwanadamu asiyeweza kutawala au kudhibiti roho ni mpumbavu katika mithali), 15:45, 16:18. Wakorintho wa pili 2:13 (kasirisha), 3:6, 6 (Kuwaza) 4:13, 7:1 (wazo). Wagalatia 6:1,18. Waefeso 1:17-18 (hekima, maarifa, na machoya kuelewa (kuona na mawazo, roho), 4:23. Wafilipi 1:27, 3:3. Wakolosai 2:5. Timotheo wa pili 1:7. Waebrania 1:7, 14, 4:12, 12:23. Yakobo

2:26, 4:5. Waraka wa kwanza wa petro 3:4. Waraka wa kwanza wa Yohana 4:1, 2, 3, 6. Kumbuka kwamba roho yako hushughulikia imani yako, fikra, welewa, mtazamo, manukato ya kihisia unayotoa wengine wakikusikiliza. Soma mara tano Wakorintho wa kwanza 2:1-3:4 na ulinganishe mtu wa kiroho (mawazo, roho, fikra) na kibinafsi (asili, hisia, ubinafsi). Fafanua Waefeso 1:15-21, 4:17-24 (kumbuka mawazo au roho katika 17, 23). Fafanua Wakorintho wa pili 2:12-17 (manukato ya kiroho kutoka agano la kale). Fafanua manukato ya uhai au kifo

**Wiki 10 Kuelewa sheria**

Kariri Warumi 6:14-15. Soma kitabu cha wagalatia,kisha mara tano Wagalatia 3:1-29 na 4:21-31 na ueleze sheria. Soma warumi 2:12-16, 3:1-31, 4:1-5 (Alikuwepo kabla ya sheria kupeanwa), Waraka wa maneno ya mitume 15:1-29 na uandike mafikio kwa maneno yako. Soma mara tatu Waebrania 8, Wakolosai 2:11-23 na ueleze. Uneza kula kivuli cha tunda? mbona sheria ikaitwa kivuli? Soma waraka wa matendo ya mitume10:1-11:17, Petro anapewa maagizo kwa njia ya Wayahudi kwa vivuli na aina zake. Ni ishara zipi ndani ya 10:11-16? Viumbe hawa wanasimamia nini ndani ya 11:18? Katika mambo ya Walawi majina ya kiebrania ya wanyama wasio safi inapeana maana. Wanyama wasio safi wana elezewa kama wa kelele nyengine ni muuaji,nyengine ni watupaji. Hawa ni kama binadamu wasio safi na wanafanya vivyo hivyo.Kama picha ya kitabu cha motto. Andika mafunzo ya Agano Jipya kuhusu Sheria. Katika Mathayo Mtakatifu 5:17-18 neno, hadi, lamaanisha nini? Je Yesu alitupilia mbaya sadaka ya kondoo au mbuzi? Hiyo ndio sheria!

**Wiki 11 Utukufu (Kihebrania: Caved, Kiyunani: Doxa)**

Kariri: Wakorintho wa kwanza 10:31, Wakorintho wa pili 1:20 (Kumbuka fasili ya Paulo). Neno lamaanisha kizito, au mzigo na inaashiria: tajiri, kumaanisha, kuwa ya maana, pole. Orodhesha njia ambazo imefafanuliwa, chopeka neno utukufu (zito), katika kila mstari katika nafasi ya utafsiri, Na toa fasili yako mwenyewe. Mwanzo 13:2, 18:20, 41:31, 43:1, 47:4, 13, Kutoka 4:10, 10, 5:9, 8:24, 9:7, 12:38, 14:4, 17, 18, 17:12, 19:16, 20:12, 34:19. Kumbukumbu la Torati 28:58. Waamuzi 1:35, 13:17, 20:34, Samweli wa kwanza 4:18, 5:6, 11, 6:6, 31:3. Samweli wa pili 6:20, 13:25. Wafalme wa kwanza 12:10, 14. Mambo ya Nyakati wa kwanza 10:3. Nehemia 5:18, Ayubu 6:3, 14:21, 23:2, 33:7. Zaburi 32:4, 38:4, 149:8 (wenye heshima). Mithali 3:9, 8:24, 27:3. Isaya 1:4, 6:10, 21:15, 24:20, 26:15, 29:13, 50:3, 59:1, 66:5, Ezekieli 27:25. Mathayo Mtakatifu 4:8, 6:13, 29, 16:27, 19:28, 24:30. Yohana Mtakatifu 2:11, 5:41, 44, 44, 7:39, 8:54, 54, 12:16, 23, 28, 28, 16:14, 17:1, 1, 4, 5, 10, 21:9. Wakorintho wa kwanza 11:7, 15:40-43. Wakorintho wa pili 3:7, 7, 8, 9, 9, Waefeso 1:6, 12, 14, 17, 18, 3:13. Wafilipi 3:19, 21. Wakolosai 1:11, 27, 27, 3:4. Yuda 8. Soma mara 2 Samweli wa kwanza 2:22-36. Utukufu kwenye mstari wa 29 (mafuta ya sadaka yalikuwa ni ya Mungu, bora ni kwanza), mstari wa 30 utukufu unatokea mara mbili, ”wale nilio na mzigo nao, wana mzigo name.” Soma mara 3 Wakorintho wa kwanza 15:35-43. Katika 41 kila kitu kina utukufu,au maelezo mazito yake: watu, ndege, matukio. Neno utukufu limetafsiriwa ini, mara 14, kwa sababu ndiyo sehemu nzito zaidi ya viungo. Kwa hivyo katika dhabihu Mungu anataka ini, au utukufu. SSoma mara 3 Wakorintho wa kwanza 10:23-11:1 na ueleze mstari wa 31. (kumbuka kwamba nyama ilikuwa ni utukufu wa chakula). Soma mara 2 Wakorintho wa pili 3-4 na ulinganishe tukufu hizo mbili.

**Wiki 12: Shetani na Mapepo**

Kariri Waraka wa kwanza wa Yohana 4:1. Jina Shetani linamaanisha kuvamia au kuzuia.umbo lake la kike latafsiriwa kama kutuhumu, kusengenya au kufitini. Neno, Ibilisi, lamaanisha kufitini au kunena kwa mielekeo miwili kwa wakati mmoja. Katika Timotheo wa kwanza 3:8-13 kumbuka 11 ambapo mfitini ni neno la Kiyunani, ’Ibilisi-kike”. Yohana Mtakatifu 8:37-47, zingatia 44. Wakorintho wa pili 11:3-4 (kudanganya kupitia kwa wahubiri), na Timotheo wa kwanza 3:11-14. Rekodi udanganyifu wa shetani katika Mwanzo 3. Nyoka ni neno la Kiebrania, Nachash, ambayo inamaanisha yenye rangi ya Shaba, lakini pia inamaanisha kutoa sauti ya mnong’ono (masengenyo!) Wakati anaponong’ona kwa mawazo au roho, anadanganya, alivyosema Yesu.Anafanya kazi katika mawazo kufanya ovu kuonekana zuri. Wakorintho wa pili 11:13-15. Ayubu 1:1-2:10, 38:7 (nyota kwenye Biblia mara nyingi ni malaika, wote, katika mstari huu inamaanisha hakukuwa na dhambi bado), 41:1-34 Joka la kilawi (wasomi wengine waamini kuwa ni shetani). Ufunuo wa yohana 12:1-13:10, 17:1-18 (Viongozi walioitesa Israeli: Misri, Babiloni, Uajemi, Ashuru, Uyunani, Roma, Roma kutoka kwa wafu). Makala mawili yananenea roho nyuma ya binadamu: Isaya 14:1-21, Ezekieli.18:1-19. Mambo ya Nyakati wa kwanza 21:1-30 shida iko katika Hesabu 1 ambapo makuhani wanahesabu watu kwa safi (unaweza pigana) au najisi (utakufa katika vita vya Mungu) na Daudi si kuhani. Kumbuka Sauli alijaribu kuwa kuhani! Waraka wa kwanza wa Yohana 5:19 (ni dhahiri kwamba mfumo wa dunia yote u katika Yule mwovu,) maneno yoyote mengine yameongezwa na watafsiri) Waefeso 2:1-2 (tunaipumua hewa yake, maoni na falsafa) 3:8-11, 6:10-20. Yakobo 3:13-18. Katika Waraka wa kwanza wa Yohana 2:12-14 unawezaje kuwa na nguvu ya kumshinda shetani? Kumbuka katika 20 watu wote wa Mungu wana upako wake kuona ukweli wake. Luka Mtakatifu 4:1-13. Ufunuo wa Yohana 20:1-10.

**Wiki 13** Rejelea kutumia karatasi zako. Tathmini ni ya hiari.

# Ushauri na Uanafunzi

Kozi hii inashughulikia vitu vyote ambavyo utakabiliana navyo kila mara katika huduma. **Zoezi:** Peana kurasa 1 au 2 kila wiki juu ya kile biblia inafundisha kwa kila mada. Haya yatajibu kuhusu: Nani, Lini, Wapi, Mbona na Vipi ya kila mada.

**Wiki1 Kutumia maandiko kurekebisha maisha**

Kariri Yohana Mtakatifu 17:17, Timotheo wa pili 3:16-17 (kwa kawaida "Mungu alipumua" alivyofanya kwa Adamu) Mathayo Mtakatifu 22:29. Soma mara 5 Yohana Mtakatifu 8:31-47. Waraka wa pili wa Petro 1:10-21 na ufuate mwongozo wa tathmini. Soma Timotheo wa kwanza 4 angalau mara 3 (mstari wa 13 kwa kusoma hadharani). Wokovu, au okoa, hapa inamaanisha kukufanya mkamilifu. Eleza jinsi maandiko yanatosheleza mahitaji wa waaminio.

**Wiki 2 Kushiriki Injili**

**(Sehemu 1)** Kariri Sheria nne za kiroho na mistari. Mungu anakujali: Yohana Mtakatifu 3:16. Sheria 2. Mwanadamu ni mwenye dhambi na ametenganishwa na Mungu: Warumi 3:23.Sheria 3. Yesu Kristo ndiye toleo la pekee kutoka kwa Mungu kwa dhambi zako: Yohana Mtakatifu 14:6. Sheria 4 Ni lazima tukiri kuwa sisi ni watenda dhambi na tumwite Yesu atusamehe: Warumi 10:9, Waefeso 2:8.

**(Sehemu 2)** Kariri Njia ya Warumi. Warumi 3:10, 3:23, 5:12, 6:23, 5:8, 10:9-10, 10:13

**(Sehemu 3)** Shiriki injili na watu wawili.

**Wiki 3 Mungu aliumba wa kike na wa kiume**

Kariri: Mathayo Mtakatifu 19:4-6, Mwanzo 2:24 (mwili na tama ni neno sawa la kiebrania) Kwa kutumia mwongozo wa tathmini, soma na uandae mafunzo ya Biblia kuhusu ndoa. Soma mara 5 Mwanzo 1:26-3:24, 5:1-2. Soma Mathayo Mtakatifu 19:10, Waefeso 5:22-6:4, Wakolosai 3:18-21, Tito 2:1-8, Waraka wa kwanza wa Petro 2:21-3:12, Timotheo wa kwanza 3:1-5, Mithali 5, 31. Soma Wimbo ulio Bora.

**Wiki 4 , 'Usafi wa mambo ya kimwili ', Talaka na kuoa ama kuolewa tena.**

Kariri mithali 6:32-33, Waebrania 13:4. Andika kurasa moja au mbili kwa maafikio yako. Ikiwa una muda soma Mithali yote na utambue mistari kuhusu mada hio. **Sehemu 1** Talaka-Mathayo mtakatifu 5:27-32, 19:1-11, Mithali 6:20-35, Malaki 2:13-16, Kumbuku la Torati 6:1-9, 7;3-4, Yoshua 23:12-13, Ezra 9:1-15, Nehemia 13:23-27. **Sehemu 2 – Kuoa au kuolewa tena-** Warumi 7:1-3, Timotheo wa kwanza 5:3-16, soma mara tatu Wakorintho wa kwanza 7. Tanbihi: "katika Bwana pekee," Wakorintho wa pili 6:14-16. **Sehemu 3 -'Usafi wa Mambo ya Kimwili'**: Waebrania 13:4, wathesalonike wa kwanza 4:1-8, Mithali 5, Wakorintho wa kwanza 7:1-5 (mstari 1 "gusa", imetumika kwenye maandiko ya kuwasha moto na kucheza muziki). Ni nini jibu la

**Wiki 5 Wakristo na pesa**

Kariri: Wafalme wa pili 4:7, Mithali 21:20

Kariri: Wafalme wa pili 4:7, Mithali 21:20. **Sehemu 1 Tabia-** soma hizi angalau mara tano: Waebrania 13:5-6, Mathayo mtakatifu 6:19-34, Wafilipi 4:4-20.Soma ,Malaki 3:7-10 (ni maandiko haya pekee yanayoruhusu kumjaribu Mungu) Soma mara 3 kitabu cha Hagai, Eleza shida na jawabu. Je jawabu lilikuwa chakula cha bure kutoka kwa kanisa? Mbona si hivyo? **Sehemu 2 Mchungaji Lipa –** soma Nehemia 13, Wakorintho wa kwanza 9:1-18, Timotheo wa kwanza 5:1-18 (heshima/taadhima yamaanisha kulipa au staha). Rekodi kile ulichobaini.

**Sehemu 3 Kutoa** - Luka Mtakatifu 21:1-4, 2, Wakorintho wa pili 8:1-12,9:6-7, Timotheo wa kwanza 6:17-19, Wakorintho wa kwanza 16:1-2. **Sehemu 4 Kuweka akiba**-Mithali 3:15, 31:10 na pia 21:10 ni nini mawe yenye thamani? Ni ya thamani kwa sababu hayapatikani kwa urahisi, au si ya kawaidaNi wakati gani mafuta huwa yenye thamani? Eleza 21:20 ambapo mafuta ilikuwa ya afya ya ngozi yako, mwangaza wa taa, na kupika. Soma Timotheo wa kwanza 5:8 (unahusisha wajane).

**Wiki 6 Usisaidie**

Kariri: Wathesalonike wa pili 3:10, Mithali 30:15 (nusu ya kwanza). Yohana Mtakatifu 12:8, Ni nani huwajali wajane Timotheo wa kwanza 5:8,16. (Sehemu 1) Soma mara 3 Wathesalonike wa pili 3:6-15. Ni nini kimeamriwa? Kila mtu lazima afanye kazi ili ale.Wacha wasafishe jingo la kanisa, au kwa njia nyingine yoyote,kabla ya kupewa. (sehemu 2) Mpango wa Mungu kwa maskini ulikuwa nini katika Mambo ya Walawi 19:9-10, 23:22. Fursa ilitolewa kwa maskini kujisaidia. Soma kitabu cha Ruthu 2 mara 2. Boazi (aliyekuwa tajiri) aliwasaidiaje wale wajane wawili? Je, aliwapa chakula au pesa za bure? aliwacha mmoja wao kushughulika ili kumsaidia mwenzake. (Sehemu 3) Soma mara 3, Timotheo wa kwanza 5 na ueleze nafasi ya kanisa katika kuwasaidia wajane na ni kwa sababu gani? Orodha ya wajane wangekuwa wake wa wahuduma waliohudumia watu wa Mungu kwa maisha yao. Wachungaji wanafaa kulipwa, iwapo kanisa litawapa wachungaji mishahara, hawaonyeshi ukarimu kwa yeyote. Soma Nehemia 13 Wahuduma wa Mungu wako wapi na ni kwa sababu gani? Eleza Mithali 13:25, 19:15, 23:2.

**Wiki 7 Machungu ya kichinichini**

Kariri: Waebrania 12:15-16. Kwa nini machungu yakaitwa mzizi? Soma Waraka wa kwanza wa Yohana 3:10-15, Yuda 5-11. Fafanua msongo wa mawazo, hasira na machungu ya Kaini katika Mwanzo 4:1-24 (soma mara 2), Waebrania 11:4. Fafanua machungu ya Esau katika Waebrania 12:12-17, Mwanzo 25:27-34, 27:1-28:9. Machungu na hasira ni shida za sisi sote. Waefeso 4:31-32, Wagalatia 5:15, Mambo ya Walawi 19:16-17, Mithali 10:12, 18, 12:16, 14:16-17, 29, 15:1, 18, 17:9, 19:11, 22:24-25, 25:28, 26:24-26, 29:22, 30:33, Wagalatia 5:19-25, Waefeso 4:26, Wakolosai 3:8, Yakobo 1:19-20, Waraka wa kwanza wa Petro 4:8. Ufunguu wa machungu ni kuweka mtu au shida juu ya orodha yako ya maombi.

**Wiki 8 Msamaha na Kukiri**

Kariri Waraka wa kwanza wa Yohana 1:9. Soma Samweli wa pili 11:1-12:25 na pia kumbuka kwamba ilikuwa karibu miezi tisa baadaye kabla ya Daudi kukiri.Soma mara 5 Zaburi 32 na 51 (unyunyizi wa damu ya pasaka). Haya ni mambo Daudi alikiri juu ya tukio hili.Eleza tajriba ya Daudi katika kuzini na mauaji.Soma pia Zaburi 876:4-7,103:8-12,Isaya 55:6-7, Mathayo mtakatifu 11:28-30.Utafanya nini wakati huwezi badilisha au kurekebisha kile ambacho umefanya?Je,Daudi angefanya nini kuzuia anguko hilo.

**Wiki9 Nidhamu ya kanisa**

Soma mara mbili Mathayo Mtakatifu 18, na kisha soma Mathayo Mtakatifu 18:15-20 mara 3 nyingine.Mstari wa 20 unazungumzia nini katika muktadha huu? Andika hatua za kukabiliana na dhambi.Eleza Luka Mtakatifu 17:1-4. Soma mara 5 Wakorintho wa kwanza 4:14-5:13 na Wakorintho wa pili 2:3-11, 13:1-10 na utumie mwongozo wa tathmini. Wahubiri wanaotenda dhambi:Soma mara 5 Timotheo wa kwanza 1:18-20 na 5:19-25 na ujibu maswali kwenye mwongozo wa tathmini.Je wahuduma hutenda dhambi bila kupata adhabu yoyote? Kwa nini Mungu alikutana na Musa katika Kutoka 4:24-26 (ishara ya tohara ni kupashwa tohara). Tazama pia Wagalatia 1:6-10. Orodhesha maonyo ya Paulo katika Wakorintho wa pili 2:3-11, 13:1-6. Soma Filemoni mara 3. Paulo alirejesha vipi watumwa waliotenda dhambi? Vitu hivi huwa vigumu lakini havifai kupuuzwa. Viongozi ambao hawawezi fanya vitu hivi hawafai kuwa viongozi. Unapokea barua kutoka kwa kiongozi ambaye anakwambia kuwa kiongozi wa kanisa amepatikana akizini na anakataa kuacha. Mwandikie barua ambayo inaanza kwa, ”Hapa ni kile Yesu na Biblia inasema ni sharti ufanye.

**Wiki 10: Uabudu sanamu na tamaa**

Kariri: Yakobo 1:12-15. Soma Yakobo 1:1-25, na kisha soma 1:12-18 angalau mara 5 (anatumia maneno ya kuwinda na kuvua) Ni hatua zipi za dhambi anazozungumza Yakobo. Kuna yeyote anayeweza kumlaumu Mungu? Jibu ni nini katika mstari wa 21, 22. Soma mara 5 Wakorintho wa kwanza 10:1-14. Mstari wa 13 unafafanuaje matukio?Ni nini cha kawaida zaidi kuliko chakula,ngono na kunung'unika? Paulo anaita nini katika mstari wa 14? Kila dhambi ni kuabudu sanamu. Ni neno lipi ambalo linajitokeza sana katika mistari 6, 11. Maji na uabudu sanamu: Soma Yeremia 2:1-13. Wanatamani maji? Wanaonea kiu mungu kuwashughulikia. Mstari wa 13 unaeleza. Maji ni ishara ya matamanio. Ni vipi neno la kiebrania la maji ya uhai limefafanuliwa katika Mwanzo 26:19. Maji haya yanatoka wapi: Ufunuo wa Yohana 22:1, 17, 21:6. Hakuna enzi inamaanisha maji. Yesu anapeana nini kutosheleza kiu cha mwanadamu: Yohana Mtakatifu 7:37-39. Mstari wa 38 ni “mtu wa ndani”. Neno hili la tumbo limetumika vipi katika Wafilipi 3:17-19, Warumi 16:17-18. Maji yako ni mungu unayeamini anaweza kutosheleza kiu chako cha maisha.Unaonea nini kiu?

**Wiki 11 Kuteseka na Kufa**

Kariri: Yohana mtakatifu 16:33, Wafilipi 1:29 (Neno la kupeana ni neno la Kiyunani la Neema). **Sehemu 1 Kuteseka** - Soma Matendo ya Mitume 14:22. Soma Warumi 7 na 8 kupitia mara 5. Rekodi mahangaiko na fafanua jibu. Toa maoni kuhusu Kutoka 4:10-12, Ayubu 29:15, Fafanua kuja kwa Yesu katika Isaya 35. Soma Yohana Mtakatifu 9, Yesu ni mwangaza wa vipofu (5), kabla ya mtu kipofu kuweza kuona Yesualiambiwa katika mstari wa 37 alikuwa tayari amemwona Bwana, hata akiwa kipofu. Mstari wa 39 watu wenye macho mazuri ni vipofu, na mtu kipofu anaweza kuona. **Sehemu 2 Kifo**-Soma mara 5 Wakorintho wa kwanza 15, Wathesalonike wa kwanza 4:13-18 Soma mara 4 Wakorintho wa pili 4-5 na ueleze ni jinsi gani aaminiye anafaa kukiona kifo. Warumi 12:15, Yohana Mtakatifu 11:25.

**Wiki 12 Wasiwasi na Imani**

Kariri: Zaburi 37:8, Mathayo Mtakatifu 6:24-25

Soma Mathayo Mtakatifu 5-7, na tena soma mara tano 6:1-15, 19-34. Maombi yetu mengi yanapaswa kufanyiwa wapi? Ni nini shida ya kuwa na shaka (katika 25). Soma Wafilipi na uandike chini kila amri. Soma mara 3 4:4-9. Ni nini jibu la wasiwasi? Soma kitabu cha Mhubiri na urekodi yote ambayo Suleimani alijaribu kufanya kutosheleza matamanio yake maishani,na alitamatisha vipi (12:13 jinsi inavyoonyeshwa katika Wakorintho wa kwanza 7:19).

**Wiki 13 Mahusiano ya Makapera**

Kariri: Mithali 30:18-19. Suleimani, Mithali na Mhubiri yameandikiwa vijana. Vitabu hivi vinastahili kusomwa ukiwa ungali kijana,kabla ya kuanza kazi au ndoa. **Sehemu 1 kuoa**-Orodhesha mwongozo katika Wakorintho wa kwanza 7:1 (Kugusa kumetumika katika kuwasha taa,na kucheza muzuki. Anamaanisha nini?) 36 (wakati ameota maua), 39, Wathesalonike wa kwanza 4:1-8, anatumia neno la kuingia katika mkataba na kuondoka katika mstari 6). Hii inaweza kuwa stakabadhi au maneno tu. **Sehemu 2 Burudani**: Vijana ni kama muziki (Maombolezo 5:14) Soma Wimbo ulio Bora na uandike njia walivyokuwa waangalifu, au kulinda, katika mahusiano yao. Katika 8:8-10 anaeleza wasichana wengine kama milango iliyo wazi na wengine kukosa milango. Ni nini mipango ya wazazi? ”Usisisimue mapenzi yangu”, kwa vitabu, filamu, mizaha au chochote kingine. Hisia zaweza kuwa za ajabu na hatari. Soma Samweli 213, Fafanua hisia za kijana huyo. Alikuwa na upenndo wa aina gani? Katika Biblia matajiri wanaoa maskini, weusi wanaoa wazungu, lakini kila mara “katika Bwana”. Je, unaamini kwambasubira yaweza kuwa hatari? Eleza. Maombolezo 3:27 (toa maoni).

**Wiki 14 Mithali ya wenye hekima**

Soma kupitia kitabu cha Mithali na tengeneza orodha ya kile kinachosemwa kuhusu: 1. Marafiki, 2. Wasichana, 3. Pesa, 4. Biashara, 5. Wazazi, 6. Mungu.

## Tabia na Mpango wa Mungu.

Peana karatasi kila wiki ambayo inauliza na kujibu Nani?Nini? Lini? Wapi? Mbona na Vipi? kwa kila somo. Kile unachojua kumhusu Mungu kutoka kwa kila somo na ujibu swali lolote katika masomo hayo.

**Wiki 1** Kariri Waraka wa kwanza wa Yohana 5:21, Isaya 29:24.
Muungu ni wazo lolote lisilo la kweli kuhusu Mungu wa kweli ambaye ni Muumba. Soma Warumi 1:18-28 angalau mara 5. Mungu hupeana wanadamu zaidi ya mara tatu katika mwili, nafsi, roho. Eleza haya kutumia mistari.Ni kitu gani wanachokijua watu wote? soma Matendo ya mitume 17:16-34 anagalau mara tano ukiandaa makala. Orodhesha mambo matano ambayo bibilia inasema Mungu yuko ndani: Waraka wa kwanza wa Yohana 1:5, 4:8, Yohana mtakatifu 4:24, Waebrania 12:29, Timotheo wa kwanza 1:17, Malaki 3:6, Ayubu 31, Ufunuo wa Yohana 15:4.

**Wiki 2** Kariri Warumi 11:36, Wakorintho wa kwanza 10:31, Waefeso 1:11, Isaya 6:3. **Utukufu** –utukufu unamaanisha uzito, angalia Wakorintho wa pili 4:17. Inaeleza tabia kuu ya kitu chochote.Inafafanuliwa nene (Samweli wa kwanza 4:18), zito(kilichojaa chochote-Mwanzo 13:2), cha maana, cha kumaanisha. Kuna neno katika "utukufu" ambayo inamaanisha "kuwa kama au fikiri," kumaanisha hatima ya kile anachofikiri mtu ndicho cha maana zaidi, au utukufu, wa kitu chochote. Utukufu ni "ini" kama sehemu nzito zaidi ya viungo vya ndani katika dhabihu soma Wakorintho wa kwanza 15:39-41 mara tano na uandae makala. Jina lingine la Mungu ni utukufu (Kutoka 33:22). Ni mzito, mwenye maana na mwenye kumaanisha. Soma na utoe maoni kuhusu utukufu katika Zaburi 19, 104, Isaya 6, Kutoka 14:4, 17. Soma Kutoka 9:16, 14:4, 33:18-34:8 na ueleze ni kwa njia gani Mungu alidhihirisha utukufu wake. Toa maoni kwa Zaburi 96:8, 66:2, 72:19, Mathayo Mtakatifu 19:28, Luka Mtakatifu 17:18. Eleza Yoshua 7:19. Soma Waefeso 1:3-14, 2:7 mara 5 na ueleze mpango wa ndani wa MunguEleza yote katika mstari wa 11. Toa maoni kwa Zaburi 33:11, Mithali 19:21, 119:89-91, Isaya 14:24, 46:10, Danieli 4:35. Je, aliamuru mpango wake wa milele? Eleza. Eleza Waraka wa kwanza wa Petro 1:20-21, na Matendo ya Mitume 2:23. Eleza Isaya 6:3 bila kutumia neno utukufu. Mungu ameumba yote kwa utukufu wake mwenyewe kudhihirika. Bila dhambi ungeiona ghadhabu ya Mungu? Haki? Rehema? Uvumilivu? Msamaha? Ushindi juu ya dhambi na mauti? Eleza.

**Wiki 3** Kariri Wakorintho wa pili 4:18, Zaburi 145:3, 139:6, Malaki 3:6. **Milele** (olam)-Katika maandiko kila mara ni neon "ambacho hakijaonekana." Has asana inatumika kwa mwanamke (olama) ambaye amefunikwa sana na huwezi ona sehemu yoyote ya mwili wake.Neno bila mwisho linaashiria bila likomo au mpaka. Mungu ana upendo usio na kikomo, haki, rehema, wema, hekima, maarifa, nguvu, neemaukamilifu, uwepo, roho. Hayapungui wala kuzidi. Ni vizuizi vipi vimejadiliwa katika: Waefeso 1:19, 2:7, 3:8, 19-20, Warumi 11:33, Zaburi 147:5, Isaya 40:25, Zaburi 145:3, Waebrania 4:13. Eleza ni kwa nini milele Mungu atabaki kuwa siri. Ni mangapi ya Mungu yatabaki kuwepo mahali pote? Eleza ni kiwango kipi cha hekima, maarifa, nguvu, haki, ukamilifu wa Mungu uko naye kila mahali? Soma Malaki 3:6 na ueleze ni mabadiliko gani yatakuwepo kwa kila yafutayo kwa ukamilifu: hekima, nguvu, uwepo, utakatifu, kufahamu maisha, utele. Kwa nini hakosi chochote, hahitaji chochote. Fafanua Warumi 1:23, Waebrania 1:12, 6:17, Zaburi 102:26-27. Orodhesha yale Mungu hawezi fanya katika Tito 1:2, Timotheo wa pili 2:13 pia Timotheo wa kwanza 6:16, Warumi 11:29, Samweli wa kwanza 15;29. Eleza ni kwa nini Mungu hakuumbwa na yeyote, anajitosheleza, utele na ukamilifu wake, kamilifu katika yeye mwenyewe. Jina lake (tabia) ni ya milele, Habakuku anasema hatua za umilele ziko katika Yeye.

**Wiki 4** Kariri Ufunuo wa Yohana 15:4, Waebrania 12:14, Matendo ya Mitume 20:28. **Sehemu 1 Utakatifu**-Soma Isaya 6:1-3, Kwa nini hawakusema: mwenye rehema, mwenye rehema, mwenye rehema? Upendo, upendo, upendo? Wa milele wa milele, wa milele? Isaya anaendelea "dunia nzima imejaa utukufu wake." Utukufu wa Mungu ni utukufu wa utele wake mwenyewe,ukamilifu wake. Wakolosai 1:19 utele wake (pleroma) ni utele wetu au ukamilifu. Mambo ya Walawi 19:2 "muwe watakatifu, kwa maana Nami ni mtakatifu." Utakatifu ni ukamilifu wa Mungu, au utele ulio ndani mwake. Wakati kila rangi zote za upinde zinaungana yanaunda mwangaza safi. Fasili hafifu: 1. SAFI: Katika maandikochafu ni takatifu, vyombo, majengo, vifaa, mavazi, chakula, mafuta, na Wakorintho wenye dhambi wanaitwa watakatifu. 2. Tenganisha: Kabla ya uumbaji, Mungu alikuwa ametenganishwa na nini? Eleza Ufunuo wa Yohana 15:4 na Waebrania 12:10 pamoja. Je, ikoje kwa malaika ambao hawajawahi kutenda dhambi? Ukamilifu na utele wa Mungu jinsi ilivyo katika Yeye, Je anayotupa hutufanya wakamilifu? Tunahitaji ukamilifu wa kila kitu alicho Mungu. Nguvu takatifu-Wafilipi 4:19, Ushirika takatifu-Waraka wa kwanza wa Yohana 1:3. Utakatifu ni utukufu wa kila kinamfanya Mungu vikiwekwa pamoja. Mungu ni mkamilifu (Mathayo Mtakatifu 5:48) Nguvu kamilifu ni nguvu takatifu, hekima kamilifu ni hekima takatifu, upendo kamilifu, uwepo, utawala, na yote mengine ni takatifu**.** **Sehemu 2-tatu-umoja** au Utatu, ni neno ambalo lilitumiwa na mwanamume aliyeitwa Turtulian katika kanisa la mwanzo kuelezea utatu wa Mungu. Mungu hafanani na chochote wala yeyote. Maandiko yanasema wanadamu hawapaswi kufanya mfano wowote kwa maana

hawajawahi kumwona na hawawezi kumwona yeye. Soma Wakorintho wa kwanza 2:11, Kutoka 15:11 na utoe maoni. Kamwe hatuwezi kumwambia Mungu kile anapaswa kuwa. Mwanadamu yu katika mfano wa Mungu na mwanadamu ni 1 Roho (mawazo), 2 Nafsi (hisia), Mwili (mwili na matamanio). Mwanadamu ni utatu. Vitu vitatu tofauti lakini mwanadamu mmoja. Soma Mathayo mtakatifu 28:19. Ubatizo unaashiria kufa na kufufuka. Ni nani aliye mfufua Yesu kutoka kwa wafu? Soma Yohana mtakatifu 2:19-21, Warumi 1:4, Matendo ya mitume 2:24. Vyote vitatu ni uzima wa milele. Vyote vitatu vinaabudiwa, vyote vitatu vinanena kuhusu "mimi" na vyote vitatu viliumba vitu vyote, vyote vitatu viliandika maandiko, vyote vitatu vinaishi ndani ya waaminio na vitawafufua, vyote vitatu vinafanya waaminio watakatifu Yohana mtakatifu 5:23 kisha mara tano soma 1:1-18 na ueleze. Andika nakala juu ya Yohana mtakatifu 5:23, Warumi 9:5, Tito 2:13, Waebrania 1:8, Waraka wa kwanza wa Yohana 5:20, Wafilipi 2:6. Agano la kale limeandikwa katika kiebrania. Neno la Mungu ni ELOHIM na ni kwa wingi, na inaashiria miungu, malaika, matajiri, waamuzi, na kila mara ni kwa wingi, isipokua kwa Mungu wa kweli ambapo kitenzi (kuelezea kitendo) ni kwa umoja "Yeye" na kila mara huwashiria mmoja. Soma Kumbukumbu la torati 6:4 "Mungu wetu ni mmoja." Malaki 1:6 (iwapo mimi ni wa Bwana." Mhubiri 12:1 "kumbuka waumba wako." Isaya 54:5 "waumbaji wako ni mume wako." Hesabu 6:24-27 "Yaweh, Yaweh, Yaweh." Isaya 6:3 "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu." Soma Wakorintho wa pili 13:14. Katika Isaya 48:16-17 ni nani aliyemtuma Yesu? Mithali 30:3-4, wakati Yesu alijidhihirisha katika agano la kale anaitwa Malaika (tarishi) wa Bwana (yaweh). Toa maoni kuhusu mwanzo 22:15-16, Kutoka 3:6, Isaya 9:6. **Sehemu 3-**Roho ni Mungu? Matendo ya mitume 5:3-4, Wakorintho wa pili 3:17. Katika Matayo mtakatifu 12:32 ni nani anayemaanisha sana kwa kulaani? Waebrania 9:14 inasema nini kumhusu. **Sehemu 4 -** toa maoni juu ya Isaya 7:14, Mathayo mtakatifu 1:23, 8:2, 9:18, 15:25, 20:20, 28:9, 28:17, Marko mtakatifu 5:6, Waebrania 1:6-8, Yohana mtakatifu 20:8, Matendo ya mitume 20:28. Mungu ametuambia kwamba yeye ni kama familia:baba,mwana na Roho mtakatifu. Neno la Roho kuwa mwenye kutuliwaza imetumika juu ya mke katika agano la kale.Ana vitu vyote ndani yake: upendo, uhusiano, na yote mengineyo. Mwenye kuoenda wengine, wala si kujipenda wenyewe

**Wiki 5** Kariri Yohana mtakatifu 4:24, Waebrania 9:14, 10:29, Yohana mtakatifu 16:13-14. Ni roho safi na hana sehemu wala mchanganyiko. Hana nywele wala ngozi.Kila kitu kumhusu cha elezea aina ya roho Aliyo. Katika Ezekieli 16 wafikiria kutumia roho yako. Isaya 40:13-28 inasema huwezi kupima roho wa Mungu (bila mpaka). Kwa hivyo katika Mungu kuna mjua yote, aliye kila mahali, mwenye nguvu, mkamilifu. Isaya 11:2, Ufunuo wa Yohana inazungumzzia roho saba za Mungu ambazo amepewa Yesu na zote zinashughulikia mawazo (saba inamaanisha kujaa, ukamilifu) basi Yohana mtakatifu 3:34 inamaanisha nini? mistari hii inafanana kwa njia gani: Waefeso 4:23, Wakolosai 1:9, Ayubu 20:3 "Roho ya uelewa wangu," Paulo anatumia mbinu sambamba za Kiyahudi akitumia Ayubu amabyo inasema kitu sawa mara mbili katika Wakorintho wa kwanza 14:15 ambapo roho na uelewa ni kitu kimoja. Mithali 29:11 "mpumbavu hunena kutokana na wingi wa roho yake (mawazo), Danieli 5:20 "Roho yake (mawazo) ilifanywa kuwa ngumu" Danieli 2:30 pia. Kwa sababu Mungu ni Roho, kila Alicho Yeye huwa mahali pote kila wakati. Yuko wapi: Mambo ya nyakati wa pili 2:6, Matendo ya mitume 17:28. Katika Mithali wepesi wa kukasirika ni Roho fupi. Uvumilivu ni roho ndefu. Kiburi kinapatikana katika roho au mawazo. Mungu ni Roho safi, hakuna sehemu, ni Yeye pekee. Ndani yake kuona, kufahamu, kugusa, kusikia, ni maneno tofauti yanayoelezea kitu kimoja. Yeye ni kila kitu kwake Yeye.Eleza ni kwa nini Mungu hana viungo vya mwili na shida ingekuwa nini iwapo angekua navyo.

**Wiki 6** Kariri Yuda 25, Ufunuo wa Yohana 1:8, Matendo ya mitume 17:28. Wakati ni sehemu ya vilivyoumbwa. Mungu hazeeki. Katika Kutoka 3:14 Yeye "NDIYE"ambayo imefafanuliwa katika ufunuo wa Yohana 1:8 (Kiebrania hakina wakati uliopita, uliopo au ujao). Umilele kila mara ni sasa na Mungu. Timotheo wa kwanza 1:17 "Mfalme wa enzi" ya mwanadamu, ambapo Waebrania 1 inasema aliumba. Soma na uorodheshe vitu vya milele vya Mungu: Warumi 1:20, Timotheo wa kwanza 6:16, Ufunuo wa Yohana 1:6, Mithali 8:23, Zaburi 33:11, 41:13, 100:5, 112:6, 132:12, 119:89, Isaya 26:4, 46:9-10, 54:8, Yeremia 10:10, 31:3, Danieli 4:3, Waraka wa pili wa Petro 3:8, Yoshua 10:12-14, Wafalme wa pili 20:1-11. Mungu haoni siku za usoni, Anaitangaza na kuiamuru. Uzima wa milele ni kuishi katika ukamilifu wa Mungu. Andaa makala kuhusu: Yohana mtakatifu 1:4, 5:26, 6:57-58, 14:6, Warumi 8:2. 2 Mungu yuko wapi: Wafalme wa kwanza 8:27, Zaburi 139, Isaya 66:1, Yeremia 23:23-24, Matendo ya mitume 7:48-49, 17:27-28. Uumbaji ni kama godoro, bahari indani yake na nje yakekwa hivyo yote ya Mungu yanajaza yote, lakini bado yako nje ya yote. 3 Ukweli: toa maoni kuhusu Waraka wa kwanza wa Yohana 5:20. Yeye pekee ndiye huona vitu vyote pamoja jinsi vilivyo kwa hivyo Warumi 3:4, Tito 1:2, Waebrania 6:18. Ukweli wote wamrudia Mungu Zaburi 31:5, 117:2, 119:60, 146:6, Yohana mtakatifu 14:6, 17, 17:17, Waraka wa kwanza wa Yohana 5:6-7.

**Wiki 7** Kariri Zaburi 147:5, Waefeso 3:20, Timotheo wa kwanza 1:17, Samweli wa kwanza 2:3. **Sehemu I Kufahamu –** sio nini, bali ni vipi Mungu anafahamu vitu vyote kwa wakati mmoja Waefeso 3:14-15. Waraka wa kwanza wa Yohana 3:20. Samweli wa kwanza 2:3 Yeye ni Mungu wa fahamu (zaidi ya 1). Toa maoni kuhusu Ezekieli 11:5 (mawazo ni neno la kiebrania roho), Mithali 15:3, Mambo ya nyakati wa kwanza 28:9, Ayubu 38:29,37, 41, Zaburi 50:11. Mungu anajua kila mawazo, malemgo, matukio, athari, hatua, nywele na yote ambayo yanaweza kujulikana. Hawezi kusahau, kukumbuka au kujifunza. Toa maoni kuhusu Kutoka 21:13, Zaburi 90:4, Waraka wa pili wa Petro 3:8, Isaya 41:21-23. Ufahamu wa mwanzo ni Mungu kujua vitu na matukio kabla ya

kuwepo au kutokea. Soma waraka wa kwanza wa Petro 1:2, 20. Soma Warumi 8:28-30, 11:2, Warumi 9:9-13 mara tatu na ueleze ni kwa njia gani Mungu hufanya chaguo. Toa maoni kuhusu Matendo ya mitume 17:26. Ni nani alimwua Yesu? Mathayo mtakatifu 17:12, Yohana mtakatifu 10:18, Luka mtakatifu 22:22, Matendo ya mitume 2:23 (Kiyunani: Hukumu yake ya mapema ni uwezo wake wa kuyaona maeno kabla ya wakati. Ni mmoja asiye na mwisho, mpango wake wa milele ungali unaendelea. Inahusisha kila sababu na athari, kila ajali,ugumu na kile wanadamu wanaita bahati. Soma Wakolosai 1:16-17 na ueleze ni wapi tufaha ilitoka na ni kwa nini tuna tufaha leo. Eleza Isaya 14:26-27, 44:7-8, 44:24-5:7, 45:21-25, 46:8-11,48:3, Danieli 4:35, Mithali 19:21, Ufunuo wa Yohana 1:1. "jua," ni neno ambalo limetumika katika Luka mtakatifu 1:34 juu ya kuwa na uhusiano wa karibu baina ya mwanamume na mwanamke. Kujua kwa mahusiano. "Adamu alimjua mkewe na akamzalia mwana." Mungu hababahatishi siku za usoni lakini anaitangaza. Je Mungu anaushikilia msimamo wa shetani? Eleza. Mambo kupangwa kwa hatima ya mtu kabla ya wakati inamaanisha "kuweka mipaka". Soma na upange mawazo yakokwa mistari ifuatayo:Yeremia 1:5, Timotheo wa kwanza 5:21 (mengine hayapo?), Matendo ya mitume 2:23, 4:28, Warumi 8:29-30, 11:2, Waraka wa kwanza wa Petro 11:20, Waefeso 1:5, 11, Wakorintho wa kwanza 2:7, Matendo ya mitume 13:48 (inahisisha njia na masharti? Eleza), Yohana mtakatifu 6:29, Waefeso 2:7-8, Warumi 12:3, Timotheo wa pili 2:25. Timotheo wa kwanza 3:3-4, Mapenzi ya Mungu ni kwamba wanadamu wa aina zote waokolewe. **Sehemu 2 Aina ya hekima -** Ni nani mtu mwenye hekima kulingana na Yakobo 3:13-18, Zaburi 147:5 inasema hekima ya Mungu ni zaidi ya tunayoweza kunena. Kando na Mungu kujua yote Mungu ni mwenye hekima na kwa hio anaelewa kila kitu. Toa maoni kwa Warumi 11:33. Maandiko ya hekima (Mithali, Mhubiri, kwa mfano) inahusu jinsi mtu anavyoenenda. Eleza Ayubu 12:13, 36:5, 38:5. Soma Zaburi 104:1-34 na ueleze ni vipi viumbe vinahitaji hekima ya Mungu. Soma Isaya 55:8-9 na ueleze Mithali 3:5-6, 9:10. Soma Warumi 16:27, Mungu ni mwenye hekima na kwa hivyo uenenda vyema impasavyo. Yeye si moumbavu. Wakorintho wa kwanza 2:7 hekima ni karama . Toa maoni kuhusu Danieli 2:20-22, Wakprintho wa kwanza 1:24, Wakolosai 2:3. Jinsi anavyoenenda mtu mwenye hekima inaonyesha kuwa anaelewa kwamba hakuna chochpte katika maisha ambacho kinaweza kukabiliwa bila hekima itokayo kwa Mungu. Hekima ya ulimwengu huu inavyosema Wakorintho wa kwanza 2, ni ya kupita (hushindwa). Hitimisho Mhubiri 12:13.

**Wiki 8** Kariri Mathayo Mtakatifu 19:26, Zaburi 22:28, 103:18. **Sehemu 1 Aina ya nguvu**- Soma Mwanzo 17:1, Luka Mtakatifu 1:37, Warumi 4:17, Waefeso 1:19 (Kufikiri kwako ni kukubwa kiasi gani?), Mathayo Mtakatifu 3:9 (anaweza?). Ayubu 10:13, Isaya 40:28, Zaburi 62:11, Danieli 4:35, Marko Mtakatifu 14:62. Iwapo yeye ni mwenye nguvu, ni nguvu zipi aliposalia nazo akiumba kila kitu? Eleza aina hii ya nguvu, (badala ya nguvu zilizoumbwa tulizo nazo). Nguvu zake ni za milele, hazifahamiki, hazijaumbwa na yeyote, zina uhai, hazibadiliki, haki, zenye rehema, upendo, hazina mwisho, takatifu, zipo kila mahali, zina hekima, zinafahamu yote, kamilifu, na mengine mengi. Hekima ya nguvu, uwepo wa nguvu, ghadhabu ya nguvu, rehema, maarifa, na mengineyo. Nguvu zote zinatoka kwake na huombwa. Anapeana ila hagawi. Hakuna anayeweza kufanya jambo lolote (hata shetani) bila nguvuza kukopwa kutoka kwake. Soma Warumi 4:17 na Waebrania 11:3, Wakolosai 1:26. Yeye pekee huumbwa kutoka kwa kisichokuwepo; ambayo ni msimamo usiojulikana kwa mitazamo yote ya kale. Hakuna kisichotokea kwa kisichokuwepo pasipo Mungu kunena. Soma Zaburi 145:3, Ayubu 36:23, Yeremia 32:17, Warumi 1:20. Unapoomba viumbe, unaona neno lake. Inakaa kwa hali ya kuumbwa kwa nguvu zinazoishikilia. Uumbaji wa Mwanzo 1 unaendelea leo kwa neno alilosema mwanzo (neno lake halijakoma). Tufaha zetu zinatoka kwa ule mti! Maji yetu yalikuwa yakitiririka pale wakati ule. Eleza Waebrania 1:3. Katika Hesabu 14 nguvu kuu zinaonekana katika uvumilivu wa Mungu kwa wengine. Akipeana rehema, na kutoangamiza wenye dhambi. **Sehemu 2 Ukuu**-Mambo ya nyakati wa kwanza 16:31. Hakuna chochote ambacho hakitawaliwi na Mungu. Waebrania 1 na Wakolosai 1:17 ni Dhahiri "ni kupitia kwake ambapo vitu vyote vinawekwa pamoja". Anaumba majira Mwanzo 8:22. Je, Mungu anaweza kufanya dhambi kwa utukufu wake? Yusufu alipataje mamlaka juu ya Misri? Nduguze walimuuza, Mke wa Potifa alimtuhumu kwa uwongo, na alikuwa kwa njia yake. Toa maoni kukusu Ezra 6:22, Mithali 21:1, ufunuo wa Yohana 17:14-17, Kumbukumbu la Torati 8:18, Isaya 10:5, Wafalme wa kwanza 22:20-23, Matendo ya Mitume 17:28. Soma Ayubu 1,2 na utoe maoni. Toa maoni kwa Mambo ya Nyakati 29:11-12, Zaburi 47:7-8. Maneno ya kimsingi ya Kiyunani yaliyotumika kwenye Biblia: (A) PANTAKRATOR - Limetumika katika Ufunuo wa Yohana 1:8, Wakorintho wa pili 6:18, PAN(ta)inamaanisha kila kitu, na KRATOR inamaanisha kudhibiti kutumia mkono. Yesu ndiye MWENYE KUDHIBITI VYOTE. (B) EPISTATES - mara 7 yote katika Luka. Katika Luka Mtakatifu 8:24 iliktumika wakati walidhani wangekufa. Inamaanisha msimamizi au mkubwa. (C) DESPOTES - Mara 7 na pamoja na neno lingine mara 12. Mtawala wa kimabavu ni mtawala asiye wa kawaida. Anayedhibiti. Imetumika pia kwa mwanamke anayetawala boma lake katika Timotheo wa kwanza 5:14 (wakati mume wake hayupo). Mungu anatawala mataifa, wanadamu, matukio, ndege, wadudu, sababu na athari, uhai na kifo. Tazama neno "wakati" katika Yuda 25 (toa maoni) Mambo ya Nyakati wa kwanza 29:11-12, Zaburi 147:4 (na Wakorintho wa kwanza 15:41). Yote kutoka kwake, Yake na kwa sababu yake. Mara 10 Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu, na mara 10 Farao akafanya hivyo. Yote ni tukio moja! Wote walifanya hivyo! Soma Mambo ya Nyakati wa kwanza 29:11, Mambo ya Nyakati wa pili 20:6, Zaburi 22:28, 24:1, 103:19, 114:3, 145:16, Ezekieli 18:4, Mathayo Mtakatifu 20:15, Ayubu 1:20-22. Wakati Ayubu alipoteza kila kitu uamuzi wake ulikuwa upi? Katika mistari ifuatayo, Mungu anatawala vipi? Matendo ya

Mitume 14:17, Mathayo Mtakatifu 5:45, Zaburu 104:14, Mathayp Mtakatifu 6:26, 30, 10:29-30, Matendo ya Mitume 17:25-26, Samweli wa kwanza 2:6-8, Mithali 16:9. Analinda watu kutokana na kutenda dhambi katika Zaburi 19:13, 33:14-15, 81:12-16, Hosea 2:6,4:17, Mathayo Mtakatifu 6:13.

**Wiki 9** Kariri Mathayo Mtakatifu 19:17. Waefeso 3:19, Warumi 11:22. **Sehemu 1 MAPENZI YAKE** - Maandiko yananena kuhusu mapenzi ya Mungu au anachotaka, anachotamani, Eleza Kumbukumbu la Torati 29:29. Wanadamu wanasema wako huru, lakini hawachagui wazazi, taifa letu, urefu au ufupi tuutakao, talanta zetu, fursa. Ninadamu anaweza kuchagua kuwa samaki au ng'ombe? Mungu anatangaza, kuruhusu, na aitumie yote kwa utukufu wake (hatuoni jinsi ilivyo), Toa maoni kuhusu Matendo ya Mitume 14:16, Zaburi 78:29, 106:15, Mwanzo 6:3, Timotheo wa pili2:14 (kwa nini Mungu hakusitisha haya?) Mwanzo 20:6. Eleza: "Hakuna anayeweza kutenda dhambi bila Mungu." na "Mungu ana deni la yeyote?" **Sehemu 2 Wema** - Mathayo Mtakatifu 19:17, 20:15, Nahumu 1:7, Zaburi33:5, 52:1, 119:68. Iwapo ni Mungu pekee ambaye ni mwema, tunaupataje wema? Kila anachofanya ni chema, takatifu, mema kamilifu, wema usiokuwa na mwisho, wema wenye nguvu, na mengineyo. NDIO MAANA ANAFANYA ANAYOFANYA, na jinsi anavyofanya. Tunaamriwa naye kumpenda, kwa sababu Yeye ni mwema na anatupenda. Soma Marko Mtakatifu 10:17-22, Mathayo Mtakatifu 19:16-26, Luka Mtakatifu 18:18-30. Swali lake "ni mema gani nianayoweza kufanya ili kupata uzima wa milele?" Angeweza kumnunua Mungu kwa pesa. Yesu alialijibu kwa maneno yake, "mwalimu mwema" mwenye mafundisho mazuri, na yule mwanamume tajiri alikataa mafunzo yake mema. Yesu alifunua kila kitukumhusu kwa mwanamume huyu. Kilikuwa nini? Yesu alimpa nini? Yesu anaangazia 6 ya amri 10 na akawacha nje "Mungu mmoja pekee," kwa hivyo peana mali yako. Ni nani aliyekuwa mungu wake? Soma Kutoka 33:1-34:9. Mungu anaelezaje uwepo wake na jina lake? **Sehemu 3 UPENDO wa Mungu** - Kuna maneno tofauti kwenye Biblia ya UPENDO**. 1. AGAPE** - Ya kawaida sana katika maandiko kumaanisha kutafuta mema kwa ajili ya mwingine. Toa maoni kukusu aMathayo Mtakatifu 5:44, 19:19. Si hisia!Mwanamume hawezi kusema kwa mwanamke, "ninakuAGAPE, Je, utakubali nikuoe?" Katika nyakati za mwisho Mathayo Mtakatifu 24:12. Waefeso 2:25. Wakorintho wa pili 9:7, Wagalatia 5:22. Toa maoni kuhusu Waebrania 12:3-11. Usio takatifu, isiyo haki si upendo wa Mungu, Ni upendo utakaohukumu wanadamu na kuwahukumu katika siku ya hudumu. Mungu anapenda haki! Zaburi 97:2 Je, upendo ni msingi? Soma Wakorintho wa kwanza 13:1-13 na utoe maoni. Je upendo unamaanisha ukosefu wa haki, kutofikiria, au kutotii? Wafilipi 1:9. Katika Warumi 5 Mungu anawapenda maadui zake hata kama atawaangamiza katika Ufunuo wa Yohana 20**. 2. PHILOS** - Hisia zinazofurahisha.Hatujaamriwa kufanya haya kwa jirani au adui zetu. Mfano wa neno hili utatafsiriwa BUSU. Toa maoni kuhusu Mathayo Mtakatifu 10:37, Yohana Mtakatifu 5:20, 16:26, Ufunuo wa Yohana 3:19 (iinaonyesha "kugoma". STERGO-Mapenzi asili au ya familia. Kuthamini kwa upendo. Inayotarajiwa nyumbani. Toa maoni kuhusu Warumi 1:31,katika siku za mwisho Timotheo wa pili 3:3. **4. EROS**-Agano la kale halitumii neno hili la ngono.Pengine kwa sababu miungu yote ya kale ilikuwa na uchafu huo waliojijali wenyewe pekee(hawakupenda binadamu)na tamaa zao.Tanbihi:Aghalabu mapendo haya yote yamechanganywa pamoja kama kitu sawa. Mungu hupenda kwa kile anaweza kutoa wala si kupokea. Mungu ni upendo, lakini hiyo si yote aliyo Mungu. Ufalme wake na upendo ni takatifu, yenye nguvu, haki, yenye rehema, na mengineyo. Kuna maoni mengi ya kutopenda kuhusu Mungu ambayo ni miungu. **Sehemu 2 Haki** - Warumi 10:1-3 wanadamu wanapata wapi kiwango cha haki? Kumbukumbu la Torati 32:4. Mungu hayuko juu ya sheria, Yeye ni sheria na kila mara anatenda haki.Haki takatifu. Mungu anawaza nini kuhusu watenda dhambi? Zaburi 7:12, 90:8, Warumi 2:6, Amosi 8:7, Zefania 3:5, Isaya 30:9-12, Nahumu 1:2-8, Mathayo Mtakatifu 7:21-23, 12:36, 13:47-50, Matendo ya Mitume 17:31, Warumi 2:16, Wakorintho wa pili 5:11.

**Wiki 10** Kariri Yakobo 2:13, Nahumu 1:2 Rehema, Upendo na Neema mara nyimgi hukanganya.**Sehemu 1 Rehema**-Rehema inapatikana katika Agano la Kale zaidi ya mara 4 jinsi ilivyo katika Agano Jipya. Katika Yohana 3:16 ni nani aliye na upendo mkuu? Je, Mungu ana deni letu la rehema? Eleza Warumi 3, 9 na Mathayo Mtakatifu 11:20-24. Eleza. Rehema na Haki zinakutana katika Yesu. Eleza Yakobo 2:13, Zaburi 89:2, 119:64, 145;8-9, Eleza ni vipi rehema ni sehemu ya neno la Mungu katika Kutoka 34:6-7. Soma Waebrania 12:29, Mambo ya Nyakati wa pili 36:5 na ueleze. Rehema zinaelezewa vipi katika Ezra 3:11, Wafalme wa kwanza 3:6, Zaburi 86:5, Luka Mtakatifu 1:78, Waraka wa kwanza wa Petro 1:3, Zaburi 103:17, Mathayo Mtakatifu 5:45, Zaburi 145:9, Matendo ya Mitume 17:25**. Sehemu 2 Uvumulivu** - Mungu aliiangamiza dunia kwa gharika. Toa maoni kuhusu Mwanzo 6:3, Waraka wa kwanza wa Petro 3:20, Ufunuo wa Yohana 2:21. Uvumilivu wa Mungu unamaanisha kwamba mwanadamu anaendelea kuchokoza. Uvumilivu ni neno la Kiebrania ni pua refu, roho ndefu, badala ya pua fupi, au roho fupi. Zaburi 145:8, Kutoka 34:6-7. Uvumilivu unahitaji nguvu kuu katika Warumi 9:22. Kisha kutokuwa na uvumilivu ni udhaifu. **Sehemu 3 Hasira, ghadhabu** - Toa maoni kuhusu Mithali 8:36, Zaburi 97:10,Waefeso 4:26(je, hasira ni dhambi?).Soma Warumi 1;16-32 na kitabu cha Nahumu na utoe maoni kwa yote mbili.Kuna aibu ya milele(kuchanganyikiwa)Yeremia 20:11,23:40 Hukumu ya milele,Danieli 12:2Aibu ya milele **.Sehemu 4 Hofu ya Mungu** - Yeye ni Mtakatifu wala si sisi. Kumbukumbu la Torati 28:58-59, Kutoka 15:11, 20:18-20, Amosi 3:8, Mhubiri 12:13, Wakorintho wa pili 5:11, Mithali 16:6, Ufunuo wa Yohana 15:11, Mambo ya Nyakati wa pili 19:7, Zaburi 19:9, Timotheo wa kwanza 5:20. Wanadamu wote wamelaaniwa na watakabiliana na Mungu. Wote wamesulubishwa na Kristo au bila Yeye. Eleza hofu na furaha pamoja, Mathayo

Mtakatifu 28:8, Zaburi 2:11. Katika Waraka wa kwanza wa Yohana 4:18-19 hofu ni kutozungumzia Mungu, lakini katika mahusiano kati yao, na neno "Mungu" haliko katika makala ya Kiyunani.Ezra 10:3, Luka Mtakatifu 12:5, Isaya 8:13-14. Soma Wakorintho wa kwanza 10:1-13 na ueleze unavyotumika kwetu.Zaaburi 99:3, 130:4, Zaburi 80:4 kukosa hofu kunaonyesha kukosa imani. Ni vitu gani VIKUU vitatu katika Marko Mtakatifu 4:35-41, na ni kichwa kipi ungepeana kwa hadithi

**Wiki 11** Kariri Waebrania 6:18, Wagalatia 3:21, Timotheo wa pili 2:13. **Sehemu 1 Neema** - Katika Biblia yako neema imetafsiriwa kwa vitu vingi: neema, huru, furaha, kufurahia, karama. peana. na zaidi. Si deni kwa vyovyote (Kutoka 33:19). Ni Mungu anayepeana katika Yakobo 1:5. Kumbukumbu la Torati 8:18, Waebrania 4:16, Waefeso 2:4-5, Warumi 8:32. Ni kupeana na sio kurudishiwa (tazama Luka Mtakatifu 6:33-36). Umenehemeshwa kuwa jinsi ulivyo na kuwa na ulicho nacho. Toa maoni juu ya neno la kiyunani "neema" katika Wafilipi 1:29, Warumi 5:2, Waefeso 2:8-9. Zaburi 145:13. Ni Muumba pekee anayeweza kupeana vitu vyote kwa watu wote. Neema ni tunachokula, kunywa, vaa, kugusa na kuskia, kuona, lengo la kuishi, tunachoweza kukifia na kutumia kufikiri. **Sehemu 2 Vikwazo** - Soma muktadha wa Samweli wa kwanza 2:30 (kwa kawaida "ingekuwa uchafuzi kwangu.") Mungu hawezi kufanya kile kilicho kinyume na tabia zake. Hana uhuru kwa mambo kama hayo. Toa maoni kwa Habakuku 1:13, Zephania 3:5, Tito 1:1-3, Waebrania 6:8, Hesabu 15:29 (kuna maneno tofauti ya kutubu), Warumi 11:29, Timotheo wa pili 2:13, Malaki 3:6. Mungu ana vikwazo katika Wagalatia 3:21, Matendo ya mitume 4:12, Mathayo mtakatifu 26:39, Waebrania 9:22, Yohana mtakatifu 3:7. Katika Zaburi 138:2 Mungu anaweza kukiuka neno lake? Hesabu 23:19-20. **Sehemu 3 Hisia –** Hakuna ubinafsi katika Mungu anapenda kile kinachofaa kupendwa na kuchukia kile kinacho faa kuchukiwa. Mathayo mtakatifu 5:44 (kama baba yako), Waefeso 4:26. Zaburi 97:10, 101:506. Eleza hasira ya Yesu na Isaya 63:9 Yeye ni Mungu aishie, na anahisi. Wafilipi 4:4 imeamriwa. Wakolosai 1:24, Waraka wa kwanza wa Petro 4:16, 19, Warumi 8:26, Yohana mtakatifu 14:27, Waefeso 4:30. Ni kwa muda gani Mungu ameumia kwa watu na kupitia watu wake? Yesu anasimama katikati ya Mungu na mwanadamu na mapendo yao yanakutana ndani yake. Warumi 12:19. Hata kama Mungu hawezi kudhurika, anaweza kuhisi. Maandiko yanatumia maneno ambayo hayamfai Mungu, bali yanamfafanua. Ni yepi: Hofu-Mwanzo 2:22-23, Kutoka 13:17, Kumbukumbu la Torati 32:27. Mwenye wivu – Kumbukumbu la Torati 6:15, 32:21. Kutubu-Mwanzo 6:6-7, Zaburi 95:10, Yeremia 15:6. Chuki-Ufunuo wa Yohana 12:6. Pia Wafalme wa kwanza 11:9, Waebrania 1:9, Isaya 63:9, Mithali 6:16, Hosea 11:8, Waraka wa pili wa Petro 3:9, Waamuzi 10:16. Ni dhambi pekee inayomfanya Mungu kuhisi uchungu angechagua kifo na kufanyika dhambi ili wengine waondoke ndani yake. Mungu ni mwenye rehema zaidi, haki, amefichika, yupo, anapendeza, mwenye nguvu, imara, asiye eleweka, asiye badilika, asiye mpya wala mzee, mfanya kazi, pumziko, mwenye kupeana, asiyekosa, mwenye kusaidia, hujaza, mpole, mkamilifu, mtakatifu, asiye na mwisho.

**Wiki 12** Kariri Waamuzi 13:17, Waraka wa pili wa Petro 1:4, Wakorintho wa kwanza 15:28, **Sehemu 1 majina** ya Mungu. Soma Waamuzi 13 na ukumbuke mstari wa 17. Kutoka 3:13 Musa anaongea na Mungu, lakini ni nini anachohitaji na mbona? Jina lamaanisha tabia, kumbuka haya katika Mithali 22:1 ambapo yamaanisha heshima. Kwa hivyo eleza Zaburi 9:10. Jina lake ni lipi katika Kumbukumbu la Torati 28:58, Zaburi 35:13, Isaya 57:15. Ana majina mengi. Mbona? Majina yote ya Kiebrania yana maana na siyo mada; yanaeleza. Soma Waraka wa kwanza wa Samweli 25:1-31 na utoe maoni kwa mstari wa 25 ambapo jina la mwanamume lamaanisha "kuwa bila maana" kwa hivo Kutoka 20:7, Isaya 63:16. Mungu hubadilisha kila mara majina ya watu wake. Ufunuo wa Yohana 2:17 yasema ni nini watu wa Mungu? Eleza. Soma Yohana mtakatifu 17:6, 26 kisha Yohana mtakatifu 1:18. Eleza Zaburi 201, 54:1, Mithali 18:10, na Mambo ya Nyakati wa kwanza 16:29. Maana ya majina yake: **1.Jina EL au Elih(im)** - Neno la kawaida lilitafsiri Mungu (mara 2,570), lakini dhahiri yamaanisha nguvu ya kutenda. Jina lake la Muumba. Pia latafsiri Malaika, Mahakimu, Wanaume wenye nguvu, au nguvu ya haki (Mwanzo31:29) Huwa yatafsiriwa kwa wingikumaanisha zaidi ya moja. Ikitumiwa kwa Mungu wa kweli huwa yatafsiriwa kama moja kwa maana kitenzi (neno linaloelezea kitendo) kila mara yamaanisha "Alitenda" Mwanzo 1:1 "Mwanzo Mungu aliumba Mbingu na Ardhi" "Yeye" ni mmoja. Toa maoni kuhusu Mwanzo 1:26. Mhubiri 12:1 inasema waumba, Isaya 6:8. Soma Kumbukumbu la Torati 6:4, Mbona Mungu anawafunza haya? **2. Jina: Theos –** Kiyunani kwa Mungu, na zizi la neno lamaanisha kuona. Tunapata neno la kiingereza la chumba cha maonyesho kutoka kwa huu mzizi. Anaona kila kitu. Soma Mithali 12:15. Macho au kuona yamaanisha mawazo au maoni kama tunavyosema "Unaonaje swala hili?" kumaanisha "unafikiriaje?" **3. Jina: El-Shaddai -** Kawaida yenye nguvu kuongeza ubora." EL ilishughulikiwa kabla, yamaanisha, nguvu. Shaddai yaonekana mara 48 kwa Mungu na mara 24 yatafsiri titi (kama titi la mama lililo na maziwa ). Wakati mwengine wingi ni wa miungu wa asili: mvua: kuzaliwa kwa motto, mimea, na kadhalika. jina la linalokaribia (au labda neno sawa) latafsiri uwanja uliopaliliwa. maana ya mzizi ya haya yote yamaanisha KUFURA. Kwa hivyo una kuzaa matunda, tele, na neno MAZIWA li katikati ya yote. Matiti ya mwanamke hutoa maziwa, mimea izalishayo huchipuka kutola ardhini, kwa hivyo Israeli inaitwa nchi itiririkayo kwa maziwa (mashamba yazaayo), na asali" (maji matamuni maoni ya Kiebrania). Maziwa na mafuta ni maneno sawa katika Kiebrania, ma na katika Kiebrania "maziwa au mwanaume mnene" latafsiriwa "mwanamume tajiri". Mwanamumew ambaye amefura kwa utajiri. Soma Mwanzo 15:1-6, Msitari wa 2 Anasema kwa kawaida "sizai matunda ." Hakuna tunda kutokana na uvimbe, udongo au mwanamume aliyejazwa na maziwa

yenye mafuta. Katika mstari wa 5 ni nini ambacho Mungu anamwambia? Soma Mwanzo 17:1-6. Msitari wa kwanza ni EL-Shaddai kumaanisha kuboresha kwa maziwa ya mafuta (kumbuka kwamba maziwa ni wazo la kufura kutokana na uzalishaji matunda). Soma Warumi 4:13-20. Ni wapi Abrahamu anaenda kupata uzalishaji wa matunda ya watoto? Kutumia Mwanzo 49:24-35 ambapo EL_Shaddai ni jina, utaelezaje hili jina? Sasa pia Mwanzo 35:9-11. Toa maoni kuhusu Isaya 60:10-16. Kumbuka: Jina hili limetafsiriwa mara nyingi kama Mwenye nguvu, ambayo mwanzoni ilitoka kwenye tafsiri ya Agano la Kale ya Kijerumani iitwayo Septuaginti, Miaka 200 kabla ya Yesu kuzaliwa. Tafsiri hili halikufanywa vyema. Bibilia ya Kilatini iliyotafsiriwa kutoka kwa Kijerumani (si Bibilia ya Kiebrania) kama yenye nguvu,na kutokea pale ilikuja kwenye Bibilia za Kiingereza. Hii si maana ya neno la Kiebrania kama mlivyoona. **4. Jina El-Elioni -** Mwanzo 14:18, Zaburi 21:7,47:2 kumaanisha kuwa juu ya kitu. Ona lile neno katika Kumbukumbu la Torati 26:19, 28:1 ambapo wanaume wako juu ya mataifa. **5. Jina: El-Olamu -** Iliyowaka. Mungu mwenye nguvu milele. Je Mungu huwa na Nguvu chache au tele? Eleza Isaya 40:28 Katika Kiebraniania neno la milele yamaanisha, kutoonekana. Ukiweka sauti-A mwisho itatafsiri kuwa mwanamwali. Hawakuonekana kwa sababu ya neti. Paulo anaeleza vipi neno katika Waraka Wakorintho wa Pili 4:17 **6. Jina:YHVH,Yahweh -** Jina hili ni herufi nne bila irabu. Hakuna mtu leo anayejua jinsi lilitamkwa. Tafsiri zengine zatumia jina Mungu katika herufi kubwa. Lakini Mungu si jina, bali mada. Yapatikana mara 6,823 na yamaanisha mmoja ambaye anapatikana ndani yake mwenyewe. Soma Kutoka 3:13-15. Je jina hilo lamaanisha nini?, katika Kiebrania, maneno yale yamaanisha, Nlikua, Niko, na Ntakuwepo. Hakuna wakati uliopita, uliopo au ujao katika Lugha ya Kiebrania. Ni nani ambaye Yesu alidai kuwa katika Ufunuo wa Yohana 1:8. Miungu wote walikua na majina katika Agano la kale na iwapo ulisema hili jina kila mtu alijua unaongelea Mungu wa Israeli. Kutoka 6:6, 43:5-7. Katika injili ya Yohana mtakatifu, Yesu anatumia, MIMI NDIMI, mara 7. Soma Mathayo mtakatifu 14:22-23 ambapo yasema "NI MIMI," lakini katika ujumbe wa Kijerumani yasomwa "Ni MIMI NDIYE" Petro anasema, "kama ndiyo," katika Kiyunani ni,"kama wewe ndiye." Hii ni, mara ya kwanza katika ambapo walimwabudu. Je walijuaje? **7. Jina: Yireh-** Soma Mwanzo 22:1-19, anamtoa mwanawe kwa siku zijazo za mahali hekalu litakalokuwa, ambapo Yesu anafia. Mstari 14 inatumia neno la, kuona, si neno la, kupeana, kupeana kwa hali ya "nitaangalia". Ni tukio lipi la kuangalia? Soma Mambo ya Nyakati wa pili 3:1. **8.Jina: Yaweh-Rafa**-Yaweh mponyaji. Soma Kutoka 15:22-27. Jina la mahali lilikuwa, "Chungu." Mstari 25 inaweza kurejelea msalaba wa Yesu. Uchungu ni uponyaji wa kwanza tunaohitaji. Hesabu 12:13, Zaburi 103:2-3, Yeremia 14:19-20.30:17, Malaki 4:2 (jua la siku ya ufufuo). **9. Jina: Yaweh-Nisi**-Kutoka 17:8-16. Yaweh fimbo yangu. Watu wangeizunguka mviringo, baadaye neno likatafsiriwa, muujiza. Fimbo hiyo ilikuwa ni ya Musa, pia inaitwa fimbo ya Aruni (mwenye mwanga) na fimbo ya Mungu. Ni fimbo iliyoota na kuzaa mlozi (imefufuka kutoka kwa wafu). Israeli wangepiga gwaride hadi kwa fimbo iliyofufuka. **10. Jina Yaweh – Mekodoshi** -Yaweh anayefanya vitu vyote vikamilifu, Mambo ya Malawi 20:7-8. Takatifu inamaanisha kuwa kamilifu. **11. Jina: Yaweh –Shalom**-Mada kuu ya Waamuzi ni "kila mtu alifanya kile alichoona haki machoni pake," na kisha katika 6:24 tuna madhabahu. SHALOM inamaanisha kulipa deni, tii kiapo, kurekebisha kilichovunjika, na kiurahisi kufanya mambo kuwa sawa. Inamaanisha amani tu kwa hali hii. Inatumika kwa mji, sadaka, tuzo, moyo, mawe, mizigo ya biashara. Hakuna kinachokosa! Eleza Zaburi 29:11, Isaya 26. **12. Jina:Y aweh sedikenu**-Yaweh Haki Yetu, katika Yeremia 23:5-6, 33:16. **13. Jina :Yaweh-Mlishaji wangu**-Zaburi 23 Mlishaji, kwa kawaida inatafsiriwa kama Mchungaji. Eleza jinsi neno, mlishaji, linaingiana na Zaburi 23. Eleza Yohana Mtakatifu 21:15-17. Kutoka 34:11-16, ni malisho mangapi? **14. Jina Yaweh-Shama** - Ezekieli 48:35 na inamaanisha Yaweh Yupo. **15. Jina Yaweh-Tsevaoti-** Yaweh wa Majeshi. Soma Wafalme wa kwanza 22:19-28, Ufunuo wa Yohana 19:14. **16. Jina: Adonai -** Kwa mara yatafsiriwa, Mungu, Mume, Bwana, Mmiliki. Yamaanisha kuwa msingi waa kubeba mzigo. **17. Jina: H-amina-**Amina na ukweli katika Kiebrania ni maneno yenye mzizi mmoja. Kile unachoweza kukiamini. Toa maoni kwa Isaya 65:16, Ufunuo wa Yohana 3:14, Hesabu 5:1-22. Wakorintho wa kwanza 14:13-16. **18. Jina: Logos -** Neno, Ujumbe, Mpango. NENO imetafsiriwa "Mtakatifu wa watakatifu" katika Wafalme wa kwanza 6:16, 19, 20, 21, 23, 31, pia 8:6, 8. Mungu wa Hekalu anaendewa kupitia kwa neno lake, nay eye ndiye NENO katika Yohana mtakatifu 1:1. **19. Sehemu 2 Utele wa Mungu -** Soma Zaburi 17:15, Waraka wa kwanza wa Yohana 3:2 na Wakorintho wa kwanza 15:28. Mwishowe tunapata utele wa Mungu. Vyote vilivyo vya Mungu vitajaza wote walio wa Mungu. Viumbe haviwezi kututosheleza kwa maana sisi ni sehemu yake.Atatupa na Kujidhihirisha kwetu milele.Milele tutajazwa na kutoshelezwa naye.

**Wiki 13 Mukhtasari wa Wiki ya mwisho**

Kutumia kile ulichosoma.Andika kurasa mbili za fasili yako kuhusu Mungu na kile unachoamini kuwa mpango wake wa milele.

**Wiki 14 Mtihani wa mwisho-** Chaguo la mwelekezi

# Kanuni za Huduma

Usijifanyie mwenyewe! Wacha Bwana akwambie! Tena, pata nani, nini, lini, wapi, kwa nini na vipi kutoka kwa Bibilia na uandike chini utakayopata. Mwishowe utaandika mwongozo wako wa kanuni za huduma.

**Wiki 1 Maswala ya Tabia**

Kariri: Timotheo wa kwanza 3:14-15, Yakobo 3:1

Soma Timotheo wa kwanza 3:1-15 mara 5. Katika mstari 7 mwenendo wa viongozi unaangaliwa. Je analipa bili? anatii neno lake? Anashughuklikia familia yake? (shetani ni mfitini). Katika 15 ona neno sawa ambalo limetafsiriwa “sharti” katika Matendo ya mitume 4:12. Lina uzito gani neno? Tabia hizi ni lazima, zinahitajika, zinadaiwa kwa kila mtu anayehudumu kanisani katika kiwango chochote. Tabia ni kitu kikuu ambacho unaleta katika huduma. Matendo ya mitume 15:36-45. Jadili Yohana –Marko na Timotheo. Ni jinsi gani dhambi inashughulikiwa na viongozi katika Wagalatia 2:11-15 (kukemea hadharani au faraghani ?), Wafilipi 4:2-3 (Majina yao yanasomwa hadharani!), Timotheo wa kwanza 1:3-4, 18:20, 5:19-22 (hadharani au faraghani?), Tito 1:10-13 Waraka wa kwanza wa Petro 5:1-4, Ufunuo wa Yohana 2:18-29. Tunaishi katika nyakati ambapo wahubiri wanapatwa katika uzinifu na kuiba kutoka kanisani (kama Yuda) Wahubiri watenda dhambi wana kemewa na kutolewa. Kiongozi wa mwisho kabla ya Yesu ako katika Kutoka 4:21-26. Soma Wifilipi 1:12-18, 2:19-22, 3:17-19 ni nini kinachosemwa kuhusu wa wahubiri? Soma Ufunuo wa Yohana mara 3, 2:1-3:22 na kumbuka jinsi Yesu alikabiliana na watu wake. Jibu kila mara ni lipi?

**Wiki 2 Lengo la Huduma**

Kariri : Wakolosai 1:28, Mathayo 5:19

**Sehemu 1 Lengo –** Ni nini lengo la huduma? Wakolosai 1:28 (watu gani?), Waefeso 4:7-16, Wagalatia 4:11, 19.

**Sehemu 2 Kufanya mkamalifu -** Soma Timotheo wa kwanza 4, mistari 12-16 orodhesha kile Paulo anamwambia kufanya. 13 ni masomo ya hadharani ya maandiko(watu hawakuwa na Bibilia)Vitu hivi vitafanyia nini kila mmoja katika 16. Kumbuka wokovu unamaanisha kufanya mkamilifu. Atafanyaje kanisa kuwa kamilifu? Ni nini kina kisiwa katika Wakolosai 4:16, (inadhaniwa kwamba Waefeso yaweza kuwa ile barua iliyotajwa), Wathesalonike wa kwanza 5:27, Ufunuo wa Yohana 1:3 (kwa kawaida “msomaji, na wote wanaosikia na pia kutenda“). Waliisomaje bibilia? Msomaji wa Bibilia ilikua nafasi rasmi katika kanisa la mwanzo na sehemu ya mafunzo ya kuwa Mhuduma. Iwapo watu hawajui maandiko, eleza ni nani wa kulaumiwa. Yesu alisema kwa viongozi, ”hamjasoma?” lakini kwa watu, “mmesikia” .Maandiko yatafanya wote Mhubiri na watu kuwa wakamilifu. Soma Yohana mtakatifu 3:9-10, Nehemia 8:1-12 (Eleza ni nini kilitokea na kwa nini). Soma mara 3 Kumbukumbu la Torati 6:1-9 (8, maandiko yanadhibiti kile mkono unafanya na yanasimama katikati ya macho na kila kitu unachoona. 9, zingatia nyumba,malango kukukumbusha unapotoka nyumbani). Ni nani atakayekuwa mdogo katika ufalme katika Mathayo mtakatifu 5:19.

**Wiki 3 Kupanda makanisa**

Kariri Tito 1:5, Matendo ya mitume 17:24. Soma Tito yote mara 2 na kisha soma 1:5-9 mara 5 na ueleze ni jinsi gani atachagua watu hawa.Katika Timotheo wa kwanza 5:17 ni nini kazi yao kanisani.Wazee wanafanya kuhubiri na kufundisha kanisani.Timotheo wa kwanza 3 ina orodha sawa kama ya Tito.Wazee wanaitwaje pale?andika mistari 1-7 kwa maneno yako mwenyewe. Neno mzee linatumikaje katika Warumi 9:12 (neno sawa!) Soma Matendo ya mitume 20:17-35 mara 5. Ana majina mawili kwa wale warejelewa. Ni nini kilichoko kwenye mistari 17,18 (wanafanya nini hapa?) Wazee huangalia, kuchunga, kuhubiri na kufundisha. Kila mara wako zaidi ya mmoja. Hapawezi tokea mzee kuwa mmoja mchungaji au mwangalizi wa kanisa. Maneno matatu yanaelezea kiongozi katika Waraka wa kwanza wa Petro 5:1-4.Roho mtakatifu anawafanya wahuduma. Ni nini mandhari ya sehemu hii? ”Nani, Nini, Lini, Wapi, Kwanini na vipi” Paulo alikua akielekea wapi na makusudi yake yalikua yepi? Luka anatoa mifano mitatu ya mafundisho ya Paulo katika Matendo ya mitume sura 13, 17 na 20. Soma na ueleze ni kwa kikundi gani kila moja wapo ya hizi zinaelekezwa? Kumbuka maneno, ”na sasa” katika Matendo ya mitume 20:22, 25 na 32. Hizi zinaonyesha mgawanyiko. Ni nini sababu ya kila mgawanyiko? Kumbuka pia ni wakati gani au kipindi kimeonyeshwa kwa vitenzi katika kila sehemu, (kama vile. Wakati uliopita, uliopo, ujao), 20:18-21, 20:22-24, 20:25-31, 20:32-35. Tengeneza orodha ya vipengele muhimu vya huduma ya Paulo katikati ya Waefeso. Ni vipengele vipi vya huduma ambavyo vinapokezwa kwa viongozi wa kanisa katika Efeso?

**Wiki 4 Mafumbo katika Huduma**

Soma Mathayo mtakatifu 13 na Marko mtakatifu 4 mara 2. Ni nini kimetabiriwa kuhusu Masihi (Kristo) katika Zaburi 78:2, Ezekieli 17:2 (Yesu alisema mada, mwana wa Adamu, ni yeye!) Kariri: Marko mtakatifu 4:9-11 (9 ni amri ya kujibiwa.), Mathayo mtakatifu 13:51 (wale wasio itaka hawaipati.) Fumbo inamaanisha, kuweka fundisho la kidunia kuambatana na ukweli wa Kimbingu ili kuonekana. 1. Soma Mathayo mtakatifu 13 na Marko mtakatifu 4 mara 5 kwa kikao kimoja. 2. Fanya mafunzo ya kimandhari katika sehemu hii, ni nini kilimfanya Yesu kutumia mafumbo (hakuwa akiyatumia kabla ya hapa), na mafumbo kwa kawaida. Orodhesha utakayopata. 3. Orodhesha mafumbo katika sehemu hizi na vipengele tofauti tofauti vya kila fumbo. 4. Soma kila fumbo kibinfsi, vipengele vyake na uangalie ujumbe wake mkuu ni upi. 5. Umejifundisha nini kwa haya mafumbo? Orodhesha matumizi ya kibinafsi ya kila fumbo yajadiliwe darasani. Katika mtazamo Fulani wa dongo, ni nini mioyo hii ya watu (ni wangapi walikua na tunda?) ni nini kilileta tofauti? Hii itakusaidia vipi kuelewa huduma? Yesu ananukuu Isaya 6, isome mara 5 na ueleze sura. Hii inaingiliana vipi na mafumbo? Eleza Mathayo mtakatifu 21:33-22:14, Marko mtakatifu 3:20-30, 12:1-12, Zaburi 118:22-23 imenukuliwa, Isome kwa mtazamo wa Yesu.

**Wiki 5 Wanafiki/ waigizaji/ Chachu**

Kariri: Luka mtakatifu 12:1. Neno la Kiyunani la mnafiki lilitumika kwa waigizaji jukwaani. Watendaji wanaoigiza mambo yasiyo ya uhalisia ya kuishi kwao. Wahubiri hufanya hivyo pia. Soma Mathayo mtakatifu 23 angalau mara 5 kwa kikao kimoja . Haya ni maneno ya mwisho ya Yesu kwa umati. Ni nini kilisababisha kukemea hadharani waandishi na mafarisayo katika sura 22? Utagundua kwamba 23:1-7 inaeleza matendo ya Wafarisayo. Orodhesha walichokuwa wakifanya. Ni vitendo gani vya Kifarisayo tunavyovifanya? Fikiria na uwe mahususi. Katika 23:13-36 Yesu anatangaza laana 7 dhidi ya Mafarisayo na waandishi wao. Ni nini hizi saba na ni vitendo gani vya kisasa vinavyofanyika leo ambavyo vinatokana na hayo? Ni kwa njia gani sisi tumekuwa wa kifarisayo? Kule kuigiza kwa Wafarisayo kulihukumiwa vipi? (Kumbuka 23:37-39 na sura 24) Ni nini lililokuwa tumaini lao la pekee? Ni kwa nini Yesu anaonya wanafunzi wake katika Mathayo mtakatifu 16:5-12, Marko mtakatifu 8:13-21, Luka mtakatifu 12:1-3. Ni nini Chachu katika Wakorintho wa kwanza 5:1-8 na shiida yake katika mstari 6 na Wagalatia 5:9. Ni kwa njia gani tutahukumiwa kwa kuigiza kwetu kwa Kifarisayo? Tutakuwaje, "waaangalifu." Tumaini letu ni nini?

**Wiki 6 Jinsi ya kuharibu mambo**

Kariri: Mistari 2 ya chaguo lako.Soma Wakorintho wa kwanza 2:1-3:17 angalau mara 5. Eleza katika 2:1-5 ujumbe wa Paulo, jinsi na matokeo. Paulo anaeleza katika 2:6-16 jinsi ukweli unatokea kwenye mawazo ya Mungu kufikia kwa mawazo yetu.Eleza mchakato huo. (Tanbihi: Sisi, inarejelea mitume ambao ni waandishi wa maandiko). Eleza katika 3:1-4 anaeleza jinsi mchakato huu wote ulivyovunjika. Ni nini? Shida? Katika 3:4-16 anarekebisha vipi mtazamo wa uwongo kuhusu uongozi? Ni vipi mchakato wa uongozi? Unajengaje kwa dhahabu, fedha, mawe yenye thamani? Soma 1:1-3:17 mara 3 zaidi na uorodheshe maonyo, amri, marekebisho na uandike chini matumizi ya binafsi kwako. Ukoje mbinafsi (mtu wa asili), aliye kimwili, na ni nini jibu katika makala? Soma 3:18-4:21 mara 5 na kwa makini eleza kimuktadha jinsi unavyoweza kuiharibu kanisa. Unatathminije kiongozi katika 4:1-5? Weka haya katika muktadha na 3:21 na ueleze. Ni vipi 4:6-13 anaongezea hoja? Katika mstari wa 6, "waliojazwa, tajiri, wafalme," inatumia falsafa ya Stoiki. Wanastoiki walifanya mabadiliko ya hisia za kimawazo kwa kurudia vitu kwa wenyewe mara kwa mara, kama, "Mimi ni mtu,mimi ni mtu, mimi ni mtu." Ni nini majukumu na matarajio katika huduma? Katika 4:14-21 ni maneno mazito ya baba kwa mwana. Ni kwa Paulo anakuwa mkali? Linganisha na 4:19-20 na sura 5. Hitimisho? Ni nini msingi wa mamlaka katika kanisa la njyumbani? Viongozi wanafanya nini kuachilia mamlaka haya?

**Wiki 7 Vipengele muhimu katika huduma**

Kariri: Mistari 2 ya chaguo lako. Wakorintho wa pili 2:12-7:1 ni tawasifu pana ya Paulo,inayoelezea vipengele muhimu za huduma yake kwa kanisa la Wakorintho.Soma sehemu hii mara 5 na utengeneze orodha ya vipengele hivyo.

**Wiki 8 Amri kwa viongozi wa Makanisa (1)**

Timotheo wa 1,2 na Tito ni makala ya Paulo yanayoelezea mambo ya kufanya kwa wahubiri wachanga. Soma Timotheo wa kwanza mara 2,andika muhtasari wa kila sura kwa maneno yako mwenyewe. Andika amri zote za yale ya kufanya au kutofanya. Tafuta maneno kama:hitaji,ni lazima, na (kuwa "___________." Soma Matendo ya Mitume 15 yote mara 2. Ni shida gani waliyokuwa wakikabiliana nayo? Andika maoni na hitimisho yako kwa maneno yako mwenyewe. Ni vitu gani vine katika mistari 4 katika mistari 19-20,wanayostahili kufanya? Unadhani kuwa maandishi ya Mitume, na viongozi wa makanisa wanaotumia maandishi hayo,yanaweza kukabili shida zinazoweza kutokea leo? Eleza maoni yako. Ni kanuni zipi za huduma ulizoweza kuzipata katika mafunzo haya?

**Wiki 9 Amri kwa Viongozi wa Kanisa (2)**

Kariri: Mistari 2 ya chaguo lako. Soma Timotheo wa pili angalau mara 3. Andika muhtasari wa kila sura, na uorodheshe amri zote za kufanya au kutofanya jambo. Tafuta maneno kama:hitaji,ni lazima, na "kuwa ________." Barua 3 ambazo zimeandikwa kwa viongozi wa makanisa yote yanaanza kwa: Neema Rehema na Amani. Lini na kwa nini viongozi wa makanisa wahitaji haya?

**Wiki 10 Amri kwa Viongozi wa Makanisa (3)**

Soma Tito mara 5na ukariri 1:2-3, na 5. Andika muhtasari wa kila sura, na uorodheshe amri zote za kutofanya au kutofanya jambo. Tafuta maneno kama: hitaji, ni lazima, na "kuwa_________." Eleza kile wanawake wazee wanayofunza,na nani. Eleza 2:1-10 kwa maneno yako mwenyewe.

**Wiki 11 Unyenyekevu wa Mitume**

Kariri Wakorintho wa pili 12:12, Marko Mtakatifu 3:14. Soma Wagalatia 1:1, Timotheo wa kwanza 1:12-17, 2:7 Paulo anifanyikaje mtume? Andika Wagalatia 1:1 kwa maneno yako mwenyewe. Kumbuka 7 "Mimi ni mtume" na 8 "Kwa hivyo nahitaji haya." Katika Wakorintho wa pili 12:12, eleza ni kwa jinsi gani kanisa inaweza kuwatambua mitume wa kweli? Walifanyikaje Mitume katika Mathayo Mtakatifu 10:1-6, 19:28, Marko Mtakatifu 3:13-19, 6:7-13, Luka Mtakatifu 6:12-16, 9:1-6, Yohana Mtakatifu 6:70. Ni nini majukumu yao katika Matendo ya Mitume 1:6-8 (Watashuhudia mafundisho yake na Ufufuo katika kila mafunzo katika Matendo ya Mitume! Si kila mtu anaweza kufanya hayo.) 1;15-26 (Ni nini kinachohitajika kujaza nafasi ya Yuda?), 6:6 wale 12 waliwekelea mikono kwa Mashemasi wa kwanza, ingawaje hakuna aliyewekelea mikono mitume, waliteuliwa na kupewa jina na Yesu mwenyewe. Soma Matendo ya Mitume 8:4-29 Mitumeiliwabidi kujiwasilisha mbele ya Mungu kabla ya Mungu kuwaruhusu Wasamaria (nusu wayahudu, nusu mataifa) kupokea Roho Mtakatifu. Soma Matendo ya Mitume 10 ambapo pia mtume ilibidi ajiwasilishe

mbele ya Mungu kabla Mungu angeruhusu mataifa wa kwanza kupokea Roho Mtakatifu. Mitume ni viunganishi vya moja kwa moja katika kuthibitisha mamlaka ya Yesu. Wakorintho wa kwanza 15:1-11. Soma Ufunuo wa Yohana 21:9-14, Katika 9 anaonyeshwa nini? Katika 10 anaona nini? Katika 14 ni nani hawa mitume 12? Ni nani hawa 12 katika Waefeso 2:19-22 (kawaida "Mitume ambao pia ni manabii"). Katika Timotheo wa kwanza 1:12-17 Paulo anajiona kwa njia gani? Kwa nini mtu aliye katika huduma ajitazame kwa namna hii.Paulo anakumbuka kutwezwa kwake na kuwa amekuwa mpumbavu anayehitaji neema na rehema. Soma Matendo ya Mitume 8:1-4, 9:1-31 andika kile unachokiona. Paulo alikuwa jasiri, lakini kwa njia mbaya. Kanisa lilimfanyia nini katika 9:30? Matokeo yalikuwa nini katika mstari 31 ya kumtuma Sauli (Paulo) nyumbani hadi Tarso? Soma Matendo ya Mitume 11:9-27 (Soma Wagalatia 1:11-24 kwa historia Fulani). Sauli (Paulo) analetwa katika huduma na wengine, badala ya kujiteua mwenyewe jinsi alivyofanya mwanzoni. Soma Matendo ya Mitume 12:25-13:12. Katika 13:9, Sauli sasa ana jina la Kilatini, Paulo; ambayo inamaanisha chache au isiyo ya maana. Unadhani ni kwa nini Sauli alibadili jina lake hadi Paulo? Ni nini kilibadilika ndani mwake? Soma Wakorintho wa pili 11:30-33, Paulo anasema akaunti ya kikapu ilikuwa wakati wa udhaifu katika maisha yake. Wanaume 12 waliteuliwa na Yesu aliyewapa jina la mitume, Nguvu za kuponya chochote na kufanya miujiza kwa sifa zao, kuwapiga watu na upofu,kuandika maandiko, na kuamuru kanisa lolote ulimwenguni ,Wathesalonike wa kwanza 2:6, Waraka wa pili wa Petro 3:2. Mungu aliwaendesha vipi mitume katika Wakorintho wa kwanza 4:9-13, 9:1-6, 12:28, 13:1. Wakorintho wa pili 11:1-15, Ufunuo wa Yohana 2:2.

**Wiki 12 Kulisha Watu**

Kariri Yohana Mtakatifu 6:35 na ueleze jinsi anavyokata njaa au kiu chake. "Maneno ninayosema kwenu ni roho na ukweli, mwili haufaidi chochote!" Kinachofurahisha kuhusu kulisha umati ni kwamba hakunaaliyeulizia chakula.Kulisha watu elfu 5 ni muujiza wa pekee ktika injili zote nne. Soma mara kadhaa Mathayo Mtakatifu 14:13-21, Marko Mtakatifu 6:30-34, 8:13-21, Luka mtakatifu 9:10-17, Yohana Mtakatifu 6:1-40. Angalia mistari ya kimsingi inayokuambia kile Yesu anafanya. Ni nani aliyeambiwa na Yesu kuwalisha? Walianza na nini? "Leta kwangu" Yesu alisema. Ni nani aliyepitisha? Yesu anafanya kupitia kwa wengine. Mambo haya na mengine mengi yako kwenye makala haya. Yesu alikuwa akifundisha nini mitume kuhusu kulisha umati? Mkate wa kimwili au kiroho? Walisherekea vipi kwa YesuUnawapatiaje mkate wa uzima ambao ulishuka kutoka mbinguni?

**Wiki 13 Mwongozo wako**

Kwa kutumia makala yako, andika mwongozo wako wa kanuni za Huduma.

**Wiki 14 Kusoma Mwongozo wako**

Iwapo una kikindi cha mjadala, basi njooni pamoja kusoma Mwongozo Kanuni za Huduma na mpate majibu yao.

Nakala Tamati: Wengi katika huduma wanatafuta utukufu wao wenyewe na wanataka kuigiza kuliko kufundisha kama Baba na kukuza watoto wazima. MWANA, lilikuwa neno la mwanafunzi katika maandiko. Yesu anatawa; a. Roho Mtakatifu hakuteswa na kufa kwa ajili yako, kumwaga damu yake kwa ajili yekoko, kwenda kaburini kwa ajili yako, kufufuka kwa ajili yako, hayupo kwenye mkonowa kiume wa babakwa ajili yakona hakukupenda kama Yesu alisema ndiye upendo mkuu zaidi ambao binadamu anaweza kuwa nao, ambao ilikuwa ni kutoa maisha yakekwa rafiki, ambayo Roho hakufanya.Yesu anatawala! Yesu ana mamalaka yote mbinguni na duniani,Roho hafanyi hivyo. Wengi wanajihusisha katika kuabudu miungu ya kufikiria kwamba hisia zao au mawazo yao ni Mungu (Ezekieli 13:3, Wakolosai 2:18-19). Hii inamaanisha kuwa wanaabudu hisia na mawazo yao. Hisia na mawazo ya binadamu sio Mungu. Hisia katika kuhubiri inaweza kuwachachawiza watu kijifunza kuhusu Yesu, Mafundisho yake kupitia kwa maandiko,na kufanywa wakamilifu. Ili macho yao yaweze kupona na kumwona katika maandiko,masikio kupona ili kumsikia kwa utiifu, mikono kupona kumfanyia kazi, miguu kupona kutembea kwa njia zake, kuvishwa na Yeye katika mawazo yao razini. Hii ndiyo iliyoangaziwa na muujiza. Wakristo halisi wameponywa ndani na wanangojea ufufuo (Warumi 8) kwa ukombozi wa mwili. Soma maandiko kwa watu na utawafanya wakamilifu,pia wewe mwenyewe. Yesu atakupenda kwa kupenda kondoo wake kwa jinsi hii.Iwapo watu hawafanyiki wakamilifu na wakomavu kwa kuhubiri maandiko safi, huduma imefeli. Yesu alisema kwanza kutafuta ufalme wa Mungu na chakula na mavazi mtaongezewa. Huduma ambazo ombaomba ni njia ya maisha, yanakubali kwamba Yesu hajawapa, jinsi alivyosema atafanya. Kuna shida mahali. Mungu ni wa kutuza wale ambao wanamtafuta kwa bidii. Using'ang'anie chakula ambacho huangamia,bali chakula ambacho hudumu hadi uzima wa milele.